# UPEMBEZWAJI WA MWANAMKE KAMA UDOKEZI WA NAFASI YA MWANAMKE KATIKA *UTENZI WA FATUMA*

**NA**

**MAINGI HANNINGTON GITONGA**

**C50/74303/2009**

**Kazi hii imewasilishwa kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya uzamili (M.A) Kiswahili Chuo kikuu Cha Nairobi.**

**NOVEMBA 2011**

University of NAIROBI Library
0496792 3

## UNGAMO

Hii ni kazi yangu binafsi na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu chochote Kile.

03/11/2011 ..................................... ..................................

Tarehe | Hannington Gitonga Maingi

Kazi hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu Cha Nairobi.

3-11-2011 ..................................... ..................................

Tarehe | Prof. K. W. Wamitila

03-11-2011 ..................................... ..................................

Tarehe | Dkt. Zaja Omboga

**SHUKURANI**

Utafiti huu umekamilika kwa juhudi kubwa na mchango wa watu wengi. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na uzima wa mwili. Shukrani za dhati nazitoa kwa wasimamizi wangu Prof K.W. Wamitila na Dkt. Zaja Omboga.

Shukrani za kipekee Ziwaendee wahadhiri wangu wa idara ya Isimu na Lugha wafuatao: Prof. Abdulaziz, Prof. Mberia, Prof. Habwe, Dkt. Mbatiah, Dkt. Buregeya, Dkt. Mukhwana, Dkt. Zaja, Bw. Mungani na Dkt.Schroeder. Utafiti huu ni matunda ya juhudi zenu.

Nawashukuru wasimamizi wa maktaba ya Jamia Mosque na hasa Bw. Ramadhan Mohammad kwa msaada wake mkubwa wa vitabu na tafsiri ya Kiarabu.

Shukrani za moyo wangu nampa mke wangu Betty Gitonga kwa mapenzi, uvumilivu na himizo alizonipa za kuendelea mbele nilipokaribia kukata tamaa. Namshukuru pia ndugu yangu Eric na marafiki wangu Benson na Muchiri kwa msaada wao na uvumilivu wao nilipokuwa nikiandika kazi hii, Mungu awabariki.

Shukrani za kindugu nawapokeza wanafunzi wenzangu: P.Thamu, J.Maobe, J.P.Warambo, P.Kamotho, L.Okombo, S.Milikau, C. Mukhata, M.Shitemi na Dada Martha Owino kwa ushirikiano wenu. Mlikuwa zaidi ya marafiki kwangu. Mola awajalie heri mpandapo ngazi hii ya maisha.

**TABARUKU**

Kwa mwanangu Levinson Mwenda

Na

Mke wangu Betty Gitonga

**YALIOMO**

Ungamo.....ii

Shukurani.....iii

Tabaruku.....iv

Yaliomo.....v

Ikisiri.....vii

**SURA YA KWANZA**.....1

1:0 Utangulizi.....1

1:1 Sababu ya kuchagua mada.....3

1:2 Tatizo la utafiti.....4

1:3 Malengo ya utafiti.....4

1:4 Nadharia tete.....5

1:5 Upeo na mipaka.....5

1:6 Yalioandikwa kuhusu somo.....5

1:7 Msingi wa kinadharia.....7

1:8 Njia za Utafiti.....9

1:9 Hitimisho.....9

**SURA YA PILI**.....11

UBABEDUME KAMA MHIMILI MKUU WA UPEMBEZWAJI WA MWANAMKE.....11

2:0 Utangulizi.....11

2:1 Dhana ya ubabedume.....11

2:2 Historia ya ubabedume.....13

2:3 Asasi ya ndoa.....21

2:4 Asasi ya dini.....24

2:5 Asasi ya Elimu.....26

2:6 Hitimisho.....27

**SURA YA TATU** .......... 29

UHAKIKI WA UTENZI WA FATUMA .......... 29

3:0 Utangulizi .......... 29

3:1 Upembezwaji wa mwanamke katika Utenzi wa Fatuma .......... 29

3:1:1 Maisha ya Fatuma Kabla ya kuolewa .......... 29

3:1:2 Kuposwa kwa Fatuma .......... 31

3:1:3 Ndoa ya Fatuma Mbinguni .......... 33

3:1:4 Ndoa ya Fatuma duniani .......... 37

3:1:5 Mahari .......... 38

3:1:6 Mwanamke na Ubikira .......... 39

3:1:7 Mwanamke kama mzazi na mlezi. .......... 42

3:2 Hitimisho .......... 45

**SURA YA NNE** .......... 46

MATUMIZI YA LUGHA KATIKA *UTENZI WA FATUMA* . .......... 46

4:0 Utangulizi .......... 46

4:1 Ishara na uashiriaji .......... 46

4:2 Sitiari .......... 47

4:2:1 Fatuma kama chombo .......... 47

4.2.2 Fatuma kama Khurulaini .......... 51

4:3 Hitimisho .......... 53

**SURA YA TANO** .......... 54

MAHITIMISHO .......... 54

Marejeleo .......... 58

**IKISIRI**

Tasnifu hii imeshughulikia upembezwaji wa mwanamke kama udokezi wa nafasi ya mwanamke katika *Utenzi wa Fatuma.*

Kazi imegawika katika sura tano. Katika sura ya kwanza, tumeshughulikia maswala ya kimsingi yanayojenga utafiti wetu kama vile: kutambulisha utafiti, sababu ya kuchagua mada, tatizo la utafiti, madhumuni ya utafiti, nadharia tete, malengo ya utafiti, msingi wa kinadharia, upeo na mipaka, yaliyoandikwa kuhusu maada yetu na njia za utafiti tulizotumia.

Katika sura ya pili, tumeshughulikia ubabedumne kama mhimili mkuu wa upembezwaji wa mwanamke. Tumeeleza historia ya ubadume kwa kuwa historia hii inatusaidia kuelewa mfumo wa ubabedume. Baada ya kueleza historia hii, tumezieleza asasi zinazochangia kuuendeleza mfumo wa ubabedume. Asasi hizi tumezitajakuwa: dini, ndoa, utamaduni na elimu.

Katika sura ya tatu, tumeuhakiki *Utenzi wa Fatuma* kwa kutumia nadharia ya ufeministi wa kirasimi. Tumethibitisha kuwa asasi za ndoa, dini , na utamaduni ndizo zinazochangia kepembezwa kwa mwanamke katika *Utenzi wa Fatuma.*

Katika sura ya nne, tumeonyesha jinsi lugha inachangia kupembezwa kwa mwanamke katika *Utenzi wa Fatuma.* Mbinu za lugha tulizozieleza ni ishara na uashiriaji na vilevile mbinu ya sitiari.

Tumetoa mahitimisho yetu katika sura ya tano.

# SURA YA KWANZA

## 1:0 Utangulizi

Mara yangu ya kwanza kuusikia *Utenzi wa Fatuma,* ilikuwa mwaka wa 2002 nilipokuwa najifunza somo la *"Pre-twentieth Swahili poetry"* katika Chuo Kikuu Cha Nairobi. Hata hivyo, sikupata fursa ya kuusoma utenzi wenyewe. Mara yangu ya pili kuusikia utenzi huu ilikuwa mwaka wa 2009 nilipojiunga na chuo hicho tena kwa masomo zaidi. Wakati huu nilipata fursa ya kuusoma utenzi huu. Mswada niliousoma ulikuwa wa Ernst Dammann. Nilipata mswada huu kutoka kwa mhadhiri wangu Dkt. Kinene wa Mutiso wakati wa mhadhara wa darasa. Huu ulikuwa utenzi wangu wa kwanza kusoma ulioandikwa na mwanamke. Nilivutiwa sana na maudhui yake. Baada ya kuusoma utenzi huu, niligundua kuwa ingawa utenzi huu unanuia kumsifu mwanamke na kumsawiri kama kielelezo cha kuigwa na wanawake wengine, mwanamke hashughulishwi na maswala ya kijamii yanayomhusu kama vile ndoa.

Utafiti huu utashughulikia upembezwaji kama udokezi wa nafasi ya mwanamke katika *Utenzi wa Fatuma.* Tumetumia neno "upembezwaji" kwa maana ya kutoshirikishwa kwa mwanamke katika maamuzi ya kijamii. Neno "nafasi" limetumiwa kwa maana ya kiwango cha kuhusishwa kwa mwanamke katika maamuzi ya kijamii.

*Utenzi wa Fatuma* ni mmoja kati ya tenzi maarufu katika fasihi ya Kiswahili zilizoandikwa kabla ya karne ya ishirini. Utenzi huu ulitungwa na Binti Said Amin bin Uthumani. Mtunzi huyu aliishi kati ya 1800 na 1900. Mtunzi huyu aliishi katika kisiwa cha Lamu katika pwani ya Kenya. *Utenzi wa Fatuma* ni hadithi ya ndoa kati ya Fatuma na Ali. Baada ya kifo cha

Khadja, Mtume Muhammad alihuzunika sana. Mzigo wa kuwalea watoto ulikuwa mzito sana kwake. Mtume alitamani sana kuona kuwa Fatuma ameolewa. Aliomba Mungu kuhusu swala hili. Fatuma alikuwa msichana mrembo mwenye tabia nzuri na sifa zake zilienea ulimwengu mzima. Watu wengi sana walifika kwa Mtume Muhammad kumposa Fatuma. Wengine walituma wajumbe kwenda kumposa Fatuma kwa niaba yao. Miongoni mwao walikuwa wafalme kutoka kila pembe ya dunia. Makafiri walijifanya kuwa wamesilimu ili posa zao zikubaliwe na Mtume. Hata hivyo, Mtume hakukubali posa yoyote ile. Alizidi kumwomba Mungu ampe mwanamume atakayemfaa Fatuma.

Ali anampenda sana Fatuma na kutamani kumwoa, lakini hamposi kwa kuwa hana mali ya kumlipia mahari. Ali anamwomba Mungu kuhusu tatizo hili kwa unyenyekevu sana. Baadaye, Mungu anajibu maombi ya Ali. Mungu anamwambia malaika Jibrili afanye matayarisho mwafaka huko mbinguni ili ndoa kati ya Ali na Fatuma iandaliwe. Jibrili anampa malaika mwenzake Ridhwan jukumu la kushughulikia matayarisho ya arusi hiyo. Matayarisho yanapokamilika, arusi inaandaliwa. Mungu anamwakilisha Fatuma naye malaika Jibrili anamwakilisha Ali. Malaika Mikaili ndiye aliyekuwa shehe wa kuiunganisha ndoa hiyo.

Baada ya arusi, Mungu anamtuma malaika Jibrili duniani kumweleza Mtume Muhammad kuhusu ndoa ya bintiye. Malaika elfu sabini wanapewa mahari kutoka mbinguni kumpelekea Mtume. Wanabeba dhahabu nyingi sana na nguo zenye thamani kubwa. Malaika Jibrili na wenzake wanapofika duniani, wanampasa Mtume habari njema walizomletea. Mtume anafurahi sana na kwenda moja kwa moja kwa bintiye kumweleza habari hizo.

Fatuma anakubali kuolewa na Ali lakini anakataa kupokea mahari aliyoletewa. Malaika Jibrili anarudi mbinguni na kumweleza Mungu yaliyotokea. Mungu anamtuma malaika Jibrili duniani tena kumuuliza Fatuma ataje mahari aliyotaka. Kupitia kwa Mtume Muhammad, Fatuma anasema kuwa, anataka kuwa shufaa wa wanawake siku ya kiama. Malaika Jibrili anarudi mbinguni na kumweleza Mungu maombi ya Fatuma. Ombi la Fatuma linakubaliwa na aya inashuka kutoka mbinguni kama hakikisho kwa Fatuma kuhusu ombi lake. Fatuma anaifunga aya hiyo kwa uzi na kuivaa shingoni kama hirizi.

Arusi kati ya Ali na Fatuma inafanyika duniani. Asubuhi, baada arusi hiyo, Ali anagundua kuwa hakuwa na chakula chochote katika nyumba yake. Anaondoka na kwenda Syria kutafuta kazi ili aweze kuikimu familia yake. Ali anafanikiwa kupata pesa na anaanza safari kurejea kwake. Njiani, anakutana na maskini na kuwapa pesa zake zote. Kimiujiza Ali anapewa ngamia kwa deni. Ali anaiuza ngamia hiyo baadaye na kupata pesa nyingi. Anapofika nyumbani, Mtume anamweleza kuwa malaika Jibrili ndiye aliyemuuzia ngamia na mnunuzi alikuwa malaika Mikaili. Ali anaandaa sherehe kubwa ya arusi. Baadaye anapeana mali yake yote kama zaka kwa maskini.

### 1:1 Sababu ya kuchagua mada

*Utenzi wa Fatuma* umemsawiri Fatuma kuwa mwanamke mwenye tabia nzuri na mtiifu. Mwanamke huyu ametukuzwa na kusawiriwa kama kielelezo cha kuigwa na wanawake wengine. Hata hivyo, mwanamke huyu hahusishwi katika maamuzi yoyote katika *Utenzi wa*

*Fatuma*. Hii ndio sababu iliyotuchochea kutathimini upembezwaji wa mwanamke katika utenzi huu.

**1:2 Tatizo la utafiti**

Dhamira ya *Utenzi wa Fatuma* ni kumtukuza mwanamke. Fatuma amesawiriwa kama mwanamke bora anayepaswa kuigwa na wanawake wengine. Ni maoni yetu kuwa mtunzi wa utenzi huu alikuwa na lengo la kuieneza dini ya Kiislamu. Hii ndio sababu anamsawiri Fatuma kama kielelezo kwa wanawake wengine. Matarajio yetu ni kuwa mwanamke huyu angehusishwa kikamilifu katika maswala yanayomzunguka katika utenzi huu. Hata hivyo, kinyume na matarajio yetu, mwanake hahusishi katika maamuzi yoyote yanayomhusu katika utenzi huu.

Utafiti huu utashughulikia upembezwaji kama udokezi wa nafasi ya mwanamke katika *Utenzi wa Fatuma.* Maswali ambayo tunajiuliza ni: Je, kwa nini mwanamke amepembezwa katika utenzi huu? Je, ubabedume unachangia vipi kumpembeza mwanamke. Aidha tunajiuliza, ni asasi zipi zinazochangia upembezwaji wa mwanamke? Swali la mwisho ambalo tunajiuliza ni je, lugha ina mchango gani katika kupembezwa kwa mwanamke?

**1:3 Malengo ya utafiti**

Lengo la kimsingi katika utafiti huu ni kushughulikia upembezwaji wa mwanamke kama udokezi wa nafasi ya mwanamke katika *Utenzi wa Fatuma.* Tutafanya hivi kwa kueleza ubabedume kuwa mhimili mkuu wa upembezwaji wa mwanamke katika *Utenzi wa Fatuma.* Tunanuia kuonyesha pia kuwa matumizi ya lugha yanachangia kujenga maudhui ya upembezwaji wa mwanamke. Katika utafiti huu, tutaonyesha ufaafu wa nadharia ya ufeministi wa kirasimi katika kuhakiki *Utenzi wa Fatuma.*

## 1:4 Nadharia tete

i) Mwanamke amepembezwa katika *Utenzi wa Fatuma.*

ii) Ubabedume ndio sababu kuu ya kupembezwa kwa mwanamke katika *Utenzi wa Fatuma.*

iii) Matumizi ya lugha katika *Utenzi wa Fatuma* yanachangia kupembezwa kwa mwanamke.

## 1:5 Upeo na mipaka

Utafiti huu utashughulikia kipengele cha maudhui kwa kuangazia swala la upembezwaji kama udokezi wa nafasi ya mwanamke katika *Utenzi wa Fatuma.* Fani itashughulikiwa pia kwa kuwa inachangia kujenga maudhui ya upembezwaji wa mwanamke katika utenzi huu. Mswada utakaotumiwa ni ule wa Ernst Dammann.

## 1:6 Yalioandikwa kuhusu somo

Udurusu wetu wa yaliyoandikwa kuhusu somo hili utajikita katika ushairi wa Kiswahili na hasa katika mashari ya kale (mashari yaliyoandikwa kabla ya karne ya ishirini). Tumeamua kuchukua msimamo huu kwa kuwa kazi tunayoishughulikia imeandikwa katika kipindi hicho. Kufanya hivi pia kutatuwezesha kushughulikia mada yetu kwa undani zaidi kwani tutajikita katika kipindi maalum.Swala la mwanamke katika mashairi ya kale limeshughulikiwa na watafiti kwa njia tofauti. Swaleh (1992) ameshughulikia maudhui katika

*Utenzi wa Mwana Kupona*. Mtafiti huyu anasema kuwa mafundisho ya dini ya Kiislamu yanamtunukia mwanamke nafasi anayostahiki katika jamii yake. Anaendelea kusema kuwa hadhi ambayo mwanamke amepewa katika jamii yake inamstahiki vilevile.

Swaleh anasema kuwa kulingana na dini ya Kiislamu, haki za mwanamume na mwanamke ni sawa ila majukumu yao yanatofautiana kulingana na maumbile yao wawili. Mtafiti huyu anaonyesha kuwa utamaduni ndio unaochangia kugandamizwa kwa mwanamke katika *Utenzi wa Mwana Kupona.* Mtafiti huyu anadai kuwa majukumu anayopewa mwanamke na jamii yake ndio yanayochangia kumdhulumu.

Kazi ya Swaleh ni muhimu katika utafiti wetu kwani itatusaidia kuelewa jinsi utamaduni unavyochangia kudhulumiwa kwa mwanamke kwa kuwa utamaduni ni asasi moja inayosaidia kuuendeleza mfumo wa ubabedume. Kazi ya Swaleh imeshughulikia utamaduni na ndoa kama asasi tofauti. Kwa maoni yetu, dini ni sehemu ya utamaduni na hivyo basi haiwezi kutenganishwa na utamaduni. Katika kazi yetu tutashughulikia asasi hizi kama zinazoingiliana na wala hatutazitenganisha.

Momanyi (1998) ameshughulikia usawiri wa mwanamke Mwislamu wa jamii ya Waswahili katika ushairi wa Kiswahili. Katika uhakiki wake, Momanyi ameshughulikia usawiri wa mwanamke katika *Utenzi wa Mwana Kupona.* Kulingana na mtafiti huyu, mwanamke amedunishwa katika utenzi huu. Momanyi anadai kuwa sababu kuu inayopelekea kudunishwa kwa mwanamke ni dini ya Kiislamu.

Kazi ya Momanyi ni muhimu katika utafiti wetu kwa sababu itatusaidia kuelewa jinsi dini inavyochangia kudunishwa kwa mwanamke. Dini ni asasi inayochangia kuendeleza mfumo wa ubabedume ambao humpembeza mwanamke.

**1:7 Msingi wa kinadharia**

Nadharia ambayo tutaitumia katika utafiti huu ni ile ya 'ufeministi wa kirasimi'. Wamitila (2003 :253) anasema, '.... ufeministi ni nadharia ambayo inapigania ukombozi wa mwanamke kutokana na pingu za kiutamaduni, kidini, kijamii, kisiasa na kiuchumi.'

Wafula na Njogu (2007 :21) wanaeleza urasimi kuwa wakati maalumu ambapo misingi ya kazi za sanaa huwekwa na kukubalika kuwa vipimo bora kwa kazi nyingine. Kwa hivyo kwa kusema kuwa tutatumia nadharia ya ufeministi wa kirasimi, tuna maana kuwa, tutazingatia sifa za nadharia ya ufeministi hasa katika kipindi ambacho tunachukulia kuwa ndipo nadharia hii ilipowekewa misingi.

Kwa mujibu wa Wamitila (2002 :157), ' Nadharia hii ilishika nguvu katika miaka ya 1960 na kuendelea kukua na kuishia kuwa muhimu katika miaka ya karibuni.' Mwandishi huyu anataja waandishi ambao wametoa mchango mkubwa katika kuiwekea nadharia hii msingi. Hawa ni, Virginia Woolf (1929) katika kazi yake, *A Room of One's Own* na Mary Wollstonecraft (1962) *A Vindication of the Rights of Women.*

Mbali na kazi hizi mbili, kazi iliyotoa mchango mkubwa zaidi katika uhakiki wa Kifeministi ni, *The Second Sex* iliyoandikwa na Simone de Beauvoir 1949. De Beauvoir alishughulikia masuala mengi yanayomhusu mwanamke katika kueleza sababu za kunyanyaswa kwa mwanamke na mwanamume. Baadhi ya masuala aliyoyashughulikia ni kama vile: Kuumbwa kwa binadamu, kukua kwake, asasi ya ndoa na uzazi. Mwandishi huyu anasema kuwa hapo zamani mwanamume alikuwa msasi aliyepata chakula chake kwa kuwawinda wanyama. Kazi

hii ilihatarisha maisha yake kwani alikabiliana na wanyama wakali waliotishia maisha yake. Mwanamke hakuweza kushiriki kazi hii kwa sababu za kimaumbile kama vile uzazi na malezi ya watoto. Asasi na sheria zilichipuka wakati mwanamume alianza shughuli za kilimo. Shughuli hizi zilimfanya amiliki ardhi. Mwanamume huyu aliona haja ya kuwarithisha wanawe ardhi hii. Hivyo basi ikaja fikira ya kumiliki mwanamke pia ili amzalie watoto watakaoendeleza kizazi chake. Kwa maoni ya De Beauvoir, hiki ndicho chanzo cha kudhibitiwa kwa mwanamke. Mwanamke akiwa msichana anaadhibitiwa na babake na udhibiti huo kupokezwa bwanake anapoolewa.

Kazi ya Betty Friedan (1963) *The Feminine Mystique* ndiyo iliyochangia pakubwa kuzuka kwa hisia za kifeministi huko Marekani. Friedan alisema kuwa maisha ya mwanamke hayakuwa yametolewa fafanuzi toshelevu na huu ndio ulikuwa msingi wa hali aliyonayo mwanamke.

Mary Ellmann (1968) *Thinking about women* aliangazia jinsi wanawake walivyokuwa wamesawiriwa vibaya na waandishi wanaume katika kazi zao. Ellmann alisema kuwa utamaduni wa magharibi katika viwango vyote umedhibitiwa na fenomena "anayoiita kufikiria katika misingi ya utambulisho wa kijinsia. " Mhakiki mwingine aliyetoa mchango mkubwa katika nadharia hii ni Kate Millet (1969) *Sexual Politics.* Anawashambulia waandishi wa kiume kwa kuwasawiri vibaya wahusika wao wa kike.

Wananadharia hii wanapinga asasi zinazochangia katika upembezwaji na udhalilizwaji wa mwanamke. Asasi hizi ni kama vile : ndoa, dini, utamaduni na elimu. Katika utafiti huu, tutatumia nadharia ya ufeministi kwa kujikita katika mawazo ya De Beauvoir katika *The*

*Second Sex* (1949) na Millet (1969) *The Sexual Politics*. Tumeziteua kazi hizi kwa kuwa tunazichukulia kuwa za kirasimi katika uhakiki wa kifeministi.

Waandishi hawa wanadai kuwa mwanamke amedhulumiwa na mwanamume. Wanasema kuwa mfumo wa ubabedume ndio unaochangia kudhulumiwa kwa mwanamke. Wanaendelea kusema kuwa asasi za ndoa, dini na utamaduni ndizo zinazochangia pakubwa kupembezwa kwa mwanamke. Maoni haya yatatusaidia kuonyesha jinsi asasi hizo zinavyochangia kupembezwa kwa mwanamke katika *Utenzi wa Fatuma.* Sifa hizi za nadharia hii zitatusaidia kushughulikia upembezwaji wa mwanamke katika *Utenzi wa Fatuma.*

## 1:8 Njia za Utafiti

Utafiti wetu ni wa kimaktaba. Utafiti huu utahusu kusoma kwa makini kazi ya Mwana Sayyid *Utenzi wa Fatuma.* Vitabu vinavyochangia mada yetu vitasomwa. Mswada ulioteuliwa ni wa Ernst Dammann. Mswada huu uliteuliwa kwa kuwa ndio mswada pekee wa *Utenzi wa Fatuma* tulioweza kuupata.

## 1:9 Hitimisho

Katika sura ya kwanza tumezungumzia maswala ya kimsingi yanayohusiana na utafiti huu. Maswala haya ni pamoja na: utangulizi wa mada, sababu za kushughulikia mada, tatizo la utafiti, nadhharia tete, upeo na mipaka, yaliyoandikwa kuhusu mada, msingi wa kinadharia na njia za utafiti zilizotumiwa katika utafiti huu.

Katika sura inayofuata, tutachunguza ubabedume kama mhimili mkuu wa upembezwaji wa mwanamke.

# SURA YA PILI

# UBABEDUME KAMA MHIMILI MKUU WA UPEMBEZWAJI WA MWANAMKE

## 2:0 Utangulizi

Katika sura ya kwanza, tumechunguza masuala ya kimsingi yanayohusiana na utafiti huu.

Katika sura hii ya pili, tatashughulikia ubabedume kama mhimili mkuu wa upembezwaji wa mwanamke. Tutafanya hivi kwa kuonyesha jinsi mfumo wa ubabedume kupitia kwa asasi kama vile: Ndoa, dini, utamadumi na elimu zinavyochangia kupembezwa kwa mwanamke. Uelewa wa mfumo wa kiubabedume utatuwezesha kutathmini *Utenzi wa Fatuma* na kutambua namna asasi tulizozitaja zinavyochangia katika kupembezwa kwa mwanamke. Kabla ya kufanya hivyo, tutatoa ufafanuzi wa dhana ya 'ubabedume'. Baada ya kufafanua dhana hii, tutaeleza historia ya ubabedume ambayo itatusaidia kuuelewa zaidi mfumo wa ubabedume ambao ni mhili mkuu wa upembezwaji wa mwanamke.

## 2:1 Dhana ya ubabedume

Ubabedume ni mfumo wa kijamii ambao unampa mwanamume mamlaka ya kumnyanyasa na kumdhulumu mwanamke. Wakati mwingine, mwanamume mwenye umri mkubwa zaidi ya wanaume wengine katika familia ndiye anayepewa wajibu wa kuwa kiongozi katika familia hiyo. Fafanuzi tofauti zimetolewa kuhusu dhana hii:

Ensaiklopedia ya Philips (2002:582) inaeleza ubabedume kuwa, "Usemi unaotumika katika mapana yake kumaanisha uongozi na akina baba au wanaume waliokomaa katika jamii."

Wamitila (2003:241) anasema, " Ni mfumo wa kijamii ambao unamtukuza mwanamume huku ukimdhalilisha au kumdunisha mwanamke."

Millet , akimnukuu Sir. Henry Maine anasema:

> Mwanamume mwenye umri mkubwa ana mamlaka kamili katika nyumba yake. Amri yake hudhihirika akiwa hai na hata anapoaga dunia. Katika familia za kale, mwanamume alikuwa na mamlaka juu ya mali yake, bibi, watoto na watumishi. (1969:34)

Moi (2002:147) akimnukuu Irigaray anayesema, "ubabedume ni nguvu ambazo haziwezi kupingwa, zinazomzuia mwanamke kujitambulisha katika jamii." Fafanuzi hizi zote zinaelekea kuliweka wazi jambo moja; ubabedume ni itikadi na imani za kijamii zinazompa mwanamume nguvu za kumtawala mwanamke. Vilevile kutokana na fafanuzi hizi, inaeleweka kuwa ubabedume husababisha kudhibitiwa kwa wanawake na wanaume. Inabainika pia kuwa mfumo wa ubabedume umekuwepo kwa muda mrefu.

Mfumo huu unampa mwanamume nguvu za kuitawala familia yake jinsi anavyotaka. Yeye ndiye mwenye mamlaka yote na hakuna mtu yeyote katika familia anayeweza kumkosoa au kukataa kutimiza matakwa yake. Mwanamume huyo anamiliki njia za uzalishaji mali, hasa ardhi na wafanyikazi. Uwezo huu unampa nguvu nyingi na kumfanya mwanamke amtegemee na hivyo basi kumsababisha mwanamke huyo kuzidi kumnyenyekea. Millet (k.h.j:33) anasema, "Ubabedume unampa mwanamume uwezo wa kumiliki mkewe na

watoto. Aidha, mfumo huu unampa mwanamume nguvu za kuwapiga wake zake na hata kuwauza."

Mwanamke hakuwa na nguvu zozote za kuweza kujikwamua kutokana na hali hii ngumu iliyomkumba. Hii ni kwa kuwa, kama anavyosema Millet, mwanamume huyo alikuwa na uwezo wa kumpiga au hata kumuuza. Ilimbidi mwanamke awe mtiifu ili asipatwe na matatizo mengi au kupigwa. Mwanamke alinyamaza, akatii na kumchukulia mawanamume kuwa kiumbe mwenye uwezo mkubwa. Nafasi ya mwanamke katika jamii ilizidi kudidimia zaidi na kufikia viwango vya chini kabisa. Millet (k.h.j:162) anasema, "ubabedume unawadhalilisha wanawake. Mwanamke anasawiriwa kwa mtazamo hasi; anaendelea kusema kuwa kiumbe asiyezungumziwa, asiyetajwa kwa jina, ni kiumbe asiyekuwa na umuhimu wowote. mwanamke anasawiriwa kuwa kiumbe duni akilinganishwa na mwanamume. Kwa jumla, ubabedume ni mfumo ambao unamnyanyaza mwanammmke.

## 2:2 Historia ya ubabedume

Kwa kuwa ubabedume ni mhimili mkuu wa upembezwaji wa mwanamke, hatuna budi kueleza historia ya ubabedume. Uelewa wetu wa historia hii, utatusaidia kuelewa namna upembezwaji wa mwanamke katika *Utenzi wa Fatuma* unavyojitokeza.

Aidha uelewa wa historia hii utatuwezesha kuelewa jinsi asasi zinazochangia kupembeza kwa mwanamke ni muhimu katika upembezwaji wake. Kwa mfano tanaweza kuelewa kuwa asasi ya ndoa inapata umuhimu wake kwa kuwa, kupitia kwa asasi hii, watoto wanazaliwa. Watoto hawa ni muhimu sana kwani wanachangia kuzalisha mtaji kwa kuwa wafanyikazi shambani. Kwa hivyo,

watoto hawa wanachangia pakubwa kuimarika kwa mfumo wa kiubabedume ambao ni mhimili mkuu wa upembezwaji wa mwanamke. Bell na Offen wanamnukuu Jacques Rousseau anayesema:

> Wanawake hawana nguvu kama wanaume na hawawezi kufanya kazi nyingi; wanapaswa kuwategemea wanaume ambao wana nguvu na bidii. Kazi ya kimsingi ya wanawake ni kuzaa watoto wengi na kuwalea vizuri chini ya uongozi wa wanaume. (1983:42)

Hata hivyo, tunatambua kuwa, hakuna historia moja ya ubabedume duniani. Jambo ambalo ni muhimu katika utafiti huu, ni kueleza historia ya mfumo wa ubabedume kwa lengo la kupata misingi ya kuelewa zaidi mfumo wa ubabedume. Tunapoielewa historia ya ubabedume tutakuwa na fursa nzuri ya kuelewa asili ya upembezwaji ambao huendelezwa na mfumo huu wa ubabendume.

Wanadamu wawili wanapokuwa pamoja, huwa wanang'ang'a na kila mmoja kujaribu kuonyesha mwenzake kuwa ana nguvu nyingi au uwezo mwingi kumshinda. Binadamu hawa wanakuwa katika mashindano ya kuthibitisha uwezo walionao. De Beauvoir anasema:

> Wanadamu wawili tofauti wanapowekwa pamoja, kila mmoja hujaribu kumtawala mwenzake. Iwapo kila mmoja wao atafaulu kutokubali kutawaliwa na mwenzake, kunazuka hali ya mvutano kati yao. Iwapo mmoja wao ana uwezo mkubwa au nguvu kumshinda mwenzake, atamdhalilisha mwenzake na kuhakikisha kuwa hali inabakia hivyo (1949:93).

Basi inaeleweka kuwa mwanamume huwania kumdhalisha mwanamke kama njia ya kuendeleza mamlaka yake juu ya mwanamke.

Kabla ya binadamu kuanza shughuli za ukulima, mwanamke na mwanamume walishiriki vita dhidi ya maadui zao. Mwanamke alipigana kwa nguvu na kwa ujasiri kama mwanamume. Hata hivyo mwanamume bado alikuwa na nguvu zaidi. Nguvu za mwanamume zilikuwa muhimu sana katika kipindi hiki alipolazimika kukabiliana na wanyama wakali nyikani. Ingawa mwanamke alipigana bila woga, uzazi, ujauzito na kupata hedhi viliwafanya wanawake washindwe kufanya kazi na hivyo kumtegemea mwanamume kuikimu familia. Mwanamke naye alilazimika kuwashughulikia watoto na hivyo kukosa muda wa kuchuma kama mwanamume.

Kwa upande wa mwanamume, mambo yalikuwa tofauti. De Beauvoir (1949:95) anasema kuwa, mwanamume aliweza kuikimu familia yake kupitia matendo yake yaliyoashiria uasili wake wa kinyama. Tangu zamani binadamu amekuwa mvumbuzi. Mwanamume alitumia vijiti kuangusha matunda kutoka kwa miti. Alitumia rungu kuwaulia wanyama. Uvumbuzi wa kutumia vijiti na rungu ulimwezesha kujiendeleza zaidi katika jamii. Ili kufanikiwa katika shughuli za uvuvi, ilimbidi mwanamume atengeneze mtumbwi kutoka kwa mti. Alipoweza kutumia mtubwi huo na kuweza kusafiri juu ya maji, aliona raha sana. Aliona kuwa nguvu zake zimezaa matunda na kumwezesha kuvumbua zaidi. Mwanamume alianza kuandaa sherehe baada ya ufanisi katika shughuli za uvuvi na usasi.

De Beauvoir (k.h.j:96) anasema kuwa maisha ya binadamu kutoka enzi za zamani yalikumbwa na hatari nyingi. Mwanamume alikabiliana na wanyama hatari katika shughuli zake za usasi. Kufaulu katika shughuli za usasi kulimfanya mwanamume ajihisi kuwa shujaa dhidi ya hatari zilizomkumba. Ukoo wake ulimheshimu sana. Mwanamume alifaulu kudhihirisha kuwa maisha ya binadamu hayapaswi kuchukuliwa kuwa ndio yenye umuhimu zaidi duniani bali binadamu anapaswa kujishughulisha na mambo muhimu ambayo yataileteа

jamii ufanisi mkubwa. Kwa upande wake, mwanamke hakuweza kujihusisha katika shughuli zenye hatari nyingi kama alivyofanya mwanamume. Hii ilikuwa pigo kwa mwanamke kwani ilidhihirika kuwa mwanamume alitofautiana na wanyama kwa kuhatarisha maisha yake na kutumia akili ili kuweza kuilea familia yake.

Maisha ya binadamu yalibadilika pale alipovumbua na kuanza kutumia vifaa (kama vile kisu) katika shughuli zake. Kwa upande mwingine mwanamke alikuwa amekazwa na shughuli za kulea watoto; hakuweza kushiriki katika uvumbuzi wa aina yoyote. Mwanamume alitia bidii ili kuhakikisha kuwa maisha yake ya baadaye yatakuwa bora zaidi. Kwa hivyo, mwanamume aliendelea na shughuli za uvumbuzi na kutalii ulimwengu, huku mwanamke akiwa amebanwa na shughuli za uzazi na malezi. Kutokana na hayo ilibidi mwanamke amtegemee mwanamume kwa chakula na mahitaji mengine. Millet ( k.h.j: 40) anasema, " Mwanamke anazidi kudhulumiwa na mwanamume kwa kuwa mfumo wa ubabedume unamfanya mwanamke amtegemee mwanamume kiuchumi." Maoni haya yanaungwa mkono na Bell na Offen (k.h.j:49) wanaosema, " Wanawake wanawategemea wanaume kwa mahitaji yao yote."

Wakati shughuli za kilimo zilipoanza binadamu hakuwa na haja tena ya kushiriki shughuli hatari kama usasi.Kwa kuwa binadamu hakushiriki tena shughuli hatari, moyo wake ulitulia. Alipata wakati wa kupumzika na kuwazia ulimwengu alimoishi. Wakati binadamu alipoanza shughuli za kilimo, hadhi ya mwanamke katika jamii ilianza kuimarika. Kuimarika kwa hadhi ya mwanamke kulitokana na umuhimu ambao watoto walikuwa nao katika kufanya kazi shambani. Watoto walifanya kazi ya kulima na kupalilia shambani na hivyo mwanamke akawa kiumbe muhimu sana kwani ndiye aliyewazaa watoto hawa. Parpart na Sticher

(1988:64) wanasema, " Wanawake wana umuhimu katika familia kwani wanawazaa watoto ambao wanasaidia kuzalisha mali kwa kulima shambani." Ardhi iliyotumiwa kuendeleza shughuli za kilimo, ilihitaji warithi na hivyo basi uzazi ukawa muhimu sana katika jamii, kwani ardhi ilichukuliwa kuwa mali ya ukoo na jamii iliishi maisha ya kijamaa. Umiliki huu wa ardhi ulileta mshikamano kati ya familia na ukoo. Ardhi ikawa muhimu sana katika kuunganisha familia na ukoo kupitia kwa urithi. Kutukuzwa kwa mababu kulianza, kwani iliaminiwa kuwa mababu hao ndio waliowarithisha wanajamii ardhi.

Watoto walichukuliwa kuwa wa mama na walipewa jina la ukoo wa mama. Watoto hawa walikuwa na haki ya kutumia ardhi kama wenzao katika ukoo ule. Watoto walirithi mali kutoka kwa mama zao. Tunaweza kusema kuwa ardhi ilimilikiwa na wanawake. Mwanamume akagundua kuwa mwanamke alikuwa na nguvu za aina fulani ambazo hazikueleweka; alizaa watoto kutokana na nguvu za kiajabu na kupanda mimea ambayo ilimea na akavuna mazao. Mwanamume alijishughulisha na kazi ya uhunzi. Alianza kutengeneza vifaa kutoka kwa chuma. Alitengeneza vifaa hivyo kwa muundo alioupendelea na kwa mikono yake mwenyewe.

Katika kufanya kazi hii, mwanamume aligundua kuwa kufaulu kwake kulitegemea bidii yake. Alipozidisha kasi kwenye fuawe yake, alimaliza kukitengeneza kifaa haraka. Mwanamume akaongeza maarifa yake katika kutengeneza vifaa. Kufaulu kwake hakukutegemea Mungu bali bidii yake. Kwa upande mwingine, mwanamke alipanda mimea, akangoja hadi ikamea, akapalilia, akaendelea kungoja tena mpaka wakati wa kuvuna. Aliwatukuza mababu zake na kuomba ili apate mavuno mazuri. Mwanamume naye akawa amegundua uwezo na nguvu yake. Akagundua kuwa mimea inaweza kumea au isimee, lakini

hakuna kitu kinachozuia kuimarika kwa vifaa vyake kwenye fuawe. Mwanamume akaanza kutumia uvumbuzi huu katika kuwazia mambo mengine ulimwenguni. Hata hivyo, hakuweza kutenganisha dhana ya Mungu na fuawe yake. Aligundua kuwa anaweza kuongeza rutuba kwenye mchanga kwa kutolima shamba lake kwa muda fulani.

De Beauvoir (k.h.j:109) anasema "kwa kuwa mwanamke hakushiriki katika kazi alizofanya mwanamume na kwa kuwa hakufikiria kama yeye, mwanamume hakumwona kama kiumbe sawa naye." Hivyo basi, mwanamke akaishia kuonekana kama kiumbe duni akilinganishwa na mwanamume. Wolf na Witke (1975:243) wanasema kuwa, " Wanawake wanachukuliwa kuwa viumbe duni wakilinganishwa na wanaume. Wanatakiwa kuwatii baba zao hadi wanapoolewa , na wanapoolewa wanatakiwa kuwatii waume wao." Mwanamume akaendelea kutumia uvumbuzi ambao alikuwa ameufanya. Alitafuta watumwa wa kumfanyia kazi shambani kwani waliweza kufanya kazi hiyo vyema zaidi kuliko mwanamke. Mwanamke akapoteza umuhimu wake wa kiuchumi katika jamii. Aliwapiga na kuwafanyisha kazi watumwa hao bila huruma. Jinsi alivyozidi kuwachapa na kuwatesa watumwa hao, ndivyo alivyojihisi kuwa na uwezo mkubwa; akawa na kiburi sana. Baadaye mwanamume huyu alimgeukia mwanamke na kumtia katika kiwango sawa na mtumwa. Jinsi alivyozidi kupata umaarufu zaidi, ndivyo hadhi ya mwanamke ilivyozidi kuzorota. .

Mwanamume alipomiliki ardhi, alimiliki pia mwanamke. Hii ni kwa kuwa alitaka wafanyikazi shambani mwake wawe milki yake. Kwa hivyo, alimfanya mke na watoto wake watumwa. Vilevile alitaka kuwamiliki watoto, ambao watarithi ardhi yake atakapoaga dunia. Millet anasema:

Mwanamume kama kiongozi wa familia yake alimmiliki bibi yake na watoto pia. Mwanamume alikuwa na uwezo wa kuwachukua watoto wake kutoka kwa mama yao. Pia aliweza kumtaliki mkewe kwa hiari au hata kumwacha mkewe na kwenda kuishi katika eneo lingine bila kumjari.

Kufikia wakati ambapo binadamu alianza kuandika sheria, mfumo wa ubabedume ulikuwa umekita mizizi na wanaume ndio walioandika sheria hizo. Si ajabu basi kuwa wanaume hao walimpa mwanamke hadhi ya chini kabisa.

Maelezo mengine ambayo yamewahi kutolewa kuhusu historia ya ubabedume ni kuwa kulikuwa na wanawake wengi katika jamii fulani na wachache katika jamii zingine. Wanaume ambao hawakupata wanawake wa kuoa katika jamii zao, walilazimika kuoa kutoka jamii jirani. Hali hii ilipelekea wanaume kufanya biashara ya kubadilishana wanawake hao kutoka jamii moja hadi nyingine. Walifanya hivi ili kuhakikisha kuwa jamii ilikuwa na wafanyikazi wa kutosha. Vilevile walitaka kuendeleza kizazi. Gerda (1986:218) anasema, Wanawake walibadilishwa kwa bidhaa kutoka kabila moja hadi nyingine kwa sababu ya umuhimu wao katika uzalishaji mali."

Jamii ambazo zilikuwa na wanawake wengi ndizo zilizokuwa na watoto wengi. Watoto hawa walikuwa hazina kubwa kwani waliweza kulima mashamba makubwa na mavuno yakawa mengi. Jamii ambazo hazikuwa na wanawake wengi hazikuweza kulima mashamba makubwa. Kwa hivyo, jamii hizi hazikuweza kutosheleza mahitaji yao ya chakula. Chakula walichokivuna kilikuwa kichache mno kwani wafanyikazi shambani walikuwa wachache.

Wakati kulipokuwa na kiangazi, jamii hizi zenye wanawake wachache zilikumbwa na njaa na watu wengi wakaaga dunia kutokana na ukosefu wa chakula. Watu waliomba chakula kutoka kwa jamii zenye wanawake wengi, zilizokuwa zimehifadhi chakula kwenye maghala kama hazina.

Katika enzi hii, mwanamke alikuwa na umuhimu mkubwa katika jamii. Ilibidi jamii zenye wanawake wachache zifanye kila jitihada ili kupata wanawake wengi ambao wangezaa watoto waliohitajika sana katika shughuli za kilimo. Jambo hili liliwafanya wanawake wabidhaishwe. Makabila yenye wanawake wengi yaliaanza kufanya biashara ya kubadilisha wanawake na bidhaa zenye thamani. Wanaume walithaminiwa kulingana na mali waliokuwa nayo na nguvu zao za uzalishaji mali. Mwanamke alibakia kuwa mali ya mwanamume na alichukuliwa kuwa nyezo ya uzalishaji mali kupitia uwezo wake wa kuzaa. Mwanamume alimdhibiti mwanamke kwani alimchukulia kuwa chombo cha uzazi ambacho kilimwezesha kupata mali kutokana na shughuli za kilimo. Mwanamume alihakikisha kuwa anamiliki mkewe, watoto na mimea yake. Aliwarithisha wanawe wa kiume ardhi yake ili waendeleze shughuli za kilimo. Ubabedume ukawa umeshika kasi.

Wanaanthropolojia wanadai kuwa ubabedume ulizuka kutokana na juhudi za binadamu za kuzalisha mali. Wanaendelea kusema kuwa jinsi mwanadamu alivyozidi kuzalisha mali ndivyo alivyopata hamu ya kubinafsisha mali yake. Hii ilipelekea binadamu kuona haja ya kumiliki mali kibinafsi na hasa ardhi. Hapo awali binadamu huyo alikuwa anafanya shughuli za usasi na hivyo basi hakukuwa na haja ya kumiliki mali. Alipoanza shughuli za

kilimo aliweza kupata muda wa kuwazia mambo mengi. Aligundua umuhimu wa mwanamke katika shughuli za kilimo na hivyo basi akafanya juhudi za kummiliki. Wavuti ya jstor inamnukuu, Hartmann anayesema:

> Ubabedume ulitokana na shughuli za uzalishaji mali. Jinsi binadamu alivyofanikiwa katika shughuli za uzalishaji mali, ndivyo alivyogundua umuhimu wa kutaalamika. Alitaalamika katika kilimo na kuanza kumiliki mali kibinafsi. Maswala haya yalitendeka wakati ambapo jamii ya binadamu ilipokuwa imeanza kutoka katika uasili wake na ikaanza kustaarabika.

Kustaarabika kwa binadamu kulitokana na maendeleo yake katika nyanja ya uzalishaji mali. Mwanamume alifanya kila jitihada kuhakikisha kuwa nguvu za uzalishaji mali (mkewe na watoto) zimo mikononi mwake. Huu ndio uliokuwa mwanzo wa ubabedume.

## 2:3 Asasi ya ndoa

Ndoa ni asasi inayoendeleza ubabedume. Asasi hii inaendeleza ubabedume kwa kuwa ndio msingi ya familia. Kupitia kwa familia, watoto wanazaliwa katika jamii na kizazi cha binadamu kinaweza kuendelea kuwepo duniani. Millet (k.h.j:33) anasema:

> Asasi kuu inayoendeleza ubabedume ni ndoa. Ndoa hupelekea kuwepo kwa familia. Familia ni kitengo muhimu katika kuimarika kwa ubabedume kwa kuwa viongozi wa familia hizo ni wanaume.

Ndoa inawezesha mfumo wa ubabedume kukita mizizi katika jamii Kwa kuwa ndiyo inapelekea kuwepo kwa familia ambapo mwanamume ndiye kiongozi. Mwanamke anapoolewa hujipata chini ya uongozi wa mwanamume. Mambo yote anayoyafanya

yanalazimika kuidhinishwa na bwanake. Ni maoni yetu kuwa kama hakungelikuwa na ndoa katika jamii, basi ubabedume haungelikuwepo. Hii ni kwa kuwa, ili mfumo wa ubabedume uimarike vizuri, ni lazima kuwe na mtawala na mtawaliwa. Kwa kutokuwa na ndoa, mwanamume hangekuwa na mtu wa kutawala, huenda mtazamo wake kuhusu wanawake ungebadilika.

Sababu nyingine ambayo inafanya asasi ya ndoa kuendeleza ubabedume ni majukumu ambayo mwanamke amepewa katika asasi hiyo. De Beauvoir (k.h.j:449) anasema:

> Asasi ya ndoa imempa mwanamke majukumu mawili muhimu. Kwanza, ni kuzaa watoto na pili ni kuhakikisha kuwa anatimiza mahitaji ya kimapenzi kwa bwanake na kuangalia nyumba yake.

Maoni haya yanaungwa mkono na Seif-al-Hatimy (1979) anayesema kuwa sababu kuu ya ndoa ni kuzaa watoto. Kulingana na maelezo haya ndoa inachangia pakubwa kuendeleza ubabedume. Mwanamke anatakiwa kukidhi mahitaji ya mwanamume ya kimapenzi na kulinda nyumba yake. Hakuna usawa wowote hapa. Huku ni kumdhulumu mwanamke, kwa nini mwanamke awe ndiye atakayekidhi mahitaji ya mwanamume? Je, hii ina maana kuwa mwanamke hana mahitaji? Kwa kusema kuwa mwanamke anapaswa kulinda nyumba, tunapaswa kuelewa kuwa jambo hilo si rahisi kwani mwanamke anatakiwa kufanya kazi nyingi sana nyumbani. Inabidi aamke mapema, aoshe, apike, na awatunze watoto vyema. De Beauvoir (k.h.j:450) anasema:

> Kazi ya mwanamke aliyeolewa ni kuosha, kupanguza vumbi, kung'arisha sakafu na kadhalika. Hata hivyo juhudi hizi za mwanamke hazifai kitu kwani uchafu daima upo.

Ndoa inaendeleza ubabedume pia kwa kuwa mara nyingi wanawake wanapoozwa hawahusishwi katika mipango ya ndoa hiyo au kuulizwa watoe maoni yao. Wanaume kutoka familia husika (familia ya mwanamke na ya mwanamume) ndio wanaoshiriki mipango ya ndoa. . De Beauvoir (k.h.j:446) anasema:

> Wakati wa kuoa, mwanamume hamposi mwanamke moja kwa moja; wanaume kutoka familia husika ndio wanaoshughulikia swala hili. Mwanamke anaishia kujipata katika familia mpya inayotawaliwa na wanaume asiowajua.

Kwa hivyo ubabedume unazidi kutawala na ndoa inaupa nguvu zaidi. Mwanamke anapojipata katika familia hiyo ngeni inayotawaliwa na wanaume wenye mamlaka kamili, hana lingine, bali kutii na kunyenyekea. Katika sherehe ya arusi miongoni mwa tamaduni kadhaa, msichana ndiye anayemshika mkono dadake na kumkabidhi kwa bwana arusi, Morgan anasema, "Katika utamaduni wa magharibi baba ndiye anayemkabidhi bwana arusi dadake. Inaaminiwa kuwa kufanya hivi kunamfanya mwanamke kuzaa watoto wa kiume." (1992:47) Kwa hivyo, ubabedume unapewa nguvu nyingi sana na asasi ya ndoa. Umuhimu wa watoto wa kiume unahimizwa kuanzia siku ya kwanza ya kuolewa kwa manamke.

Asasi ya ndoa pia inasaidia kuendeleza mfumo wa ubabedume kwa kumfanya mwanamke mtumwa wa mwanamume. Mwanamke analazimika kumtegemea mwanamume kiuchumi kwani hapewi nafasi yoyote ya kujitafutia mali yake. Kama tulivyoeleza hapo juu mwanamke anawajibika kukaa nyumbani na shughuli zake zote ni za nyumbani. Mwanamume ndiye mwenye uwezo wa kiuchumi. De Beauvoir (k.h.j:132) anasema, "Katika

ndoa mwanamke anapigwa na tabia yake inachunguzwa kwa makini. Jinsi mwanamume anavyokuwa tajiri, ndivyo mwanamke anavyomtegemea zaidi." Mtegemea cha nduguye hufa maskini. Hivyo basi, asasi ya ndoa inapomfanya mwanamke amtegemee mwanamume, inazidi kuupa mfumo dhalilishi wa ubabedume nguvu zaidi. Mwanamke anazidi kuingia katika shimo ambalo kimo chake hakijulikani.

**2:4 Asasi ya dini**

Dini ni asasi ambayo inachangia pakubwa katika kuendeleza mfumo wa kibabedume. Dini hufanya hivi kwa kumpa mwanamume mamlaka halisi kama kiongozi wa familia yake. Millet (k.h.j:33) anasema:

> Ushirikiano kati ya familia na jamii kwa jumla ni muhimu katika mfumo wa kibabedume. Hii imepelekea jamii kuunga mkono misimamo ya kidini kama ile ya dini ya kikristo kuwa mwanamume ndiye kiongozi wa familia yake.

Mtaalamu huyu anaendelea kufafanua jambo hili zaidi kwa kusema kuwa, ubabedume unaungwa mkono na Mungu. Mafundisho ya kidini huchangia pakubwa kuupa nguvu mfumo wa ubabedume. Mafundisho hayo ya kidini humsawiri mwanamke kama kiumbe hatari na asili ya maovu yote.

Dini, hivyo basi, inasaidia sana kuendeleza mfumo wa ubabedume. Tumeeleza kuwa dini inahusu imani. Washika dini fulani huzingatia maandiko matakatifu ya dini yao bila kupinga jambo lolote. Mtu ambaye anapinga mafundisho ya dini fulani husemekana kuwa amepoteza njia. Kwa hivyo, dini inapofundisha kuwa mwanamume ndiye kiongozi wa familia, wafuasi

wake hawana budi bali kufuata na kutekeleza mafundisho hayo. Mwanamke anapojaribu kujikwamua kutokana na dhuluma ya bwanake, hukumbushwa kuwa dini inafundisha kuwa mke amtii mumewe. Mwanamke hulazimika kumtii mumewe kwa kuchelea kuwa iwapo hatamtii, atasemekana kuwa hafuati mafundisho ya kidini. Kama tulivoeleza hapo awali kuhusu historia ya ubabedume, ubabedume ulikuwa umeimarika kikamilifu kufikia wakati ambapo binadamu aligundua hati ya kuandika. Kwa hivyo, maandishi mengi kuhusiana na dini, yaliandikwa na wanaume. Dini iliupa ubabedume nguvu nyingi na mwanamke akadhalilishwa zaidi na zaidi.

Taswira ya mwanamke katika dini kadhaa inadhihirisha jinsi mwanamke alivyopembezwa. Hivi ndivyo hali ilivyo katika dini ya Kiislamu. Kurani Takatifu inasema:

> Na waambieni waaminio wanawake wainamishe macho yao, na wazilinde tupu zao, wala wasidhihirishe mapambo yao isipokuwa yale yaliyodhihirika katika hayo. Ila kwa waume wao au baba yao au baba ya waume wao, au wana wao, au wana wa waume wao, au kaka yao, au wana wa kaka yao, au wana wa dada yao, au wanawake wao, au wale iliyowamiliki mikono yao ya kuume, au watu wafikao mara kwa mara wasio watamanifu katika waume, au watoto ambao hawajajua siri za wanawake, wala wasipige miguu yao ili wajulikane wanayoyaficha katika mapambo yao. Na tubieni nyote kwa Mwenyezi Mungu, enyi waaminio, ili mpate kufaulu. (Sura 24:32)

Mwanamke amepembezwa kiasi cha kuwekewa mipaka ya nini la kufanya, kipi cha kuvaa, namna ya kutembea na kadhalika. Mambo haya yote yanadhihirisha jinsi dini inavyochangia kuendeleza ubabedume. Maoni haya ya asasi ya dini kuchangia katika kuendeleza ubabedume yameungwa mkono na De Beauvoir (k.h.j:128) anayesema:

> Mafundisho ya dini ya kikristo yamechangia kuendeleza ubabedume. Katika agano jipya, Paulo alifunza kuwa mwanamke aliumbwa ili kumtumikia mwanamume.

Dini inachangia kuendeleza mfumo wa ubabedume pia kwa kuidhinisha asasi ya ndoa ambayo kama tulivyoeleza hapo juu, imechangia sana kuupa nguvu mfumo huu wa ubabedume. Zeba anasema:

> Dini ya Kiislamu hushikilia kuwa, ndoa ni asasi ya kijamii na Waislamu wote ni lazima waoe au waolewe isipokuwa kama wana matatizo ya kiafya au matatizo mengine muhimu yanayowazuia (1976:35).

Wanawake wanapoolewa wanajipata katika familia zinazotawaliwa na wanaume. Kwa hivyo dini inachangai kuwepo kwa ubabedume kwa kuhimiza waumini wake waoe au waolewe. Watu wanatii dini zao ili kupata ufalme wa milele baada ya kifo na hivyo basi kuoa au kuolewa. Jinsi asasi ya ndoa inavyozidi kuimarika kupitia kwa asasi ya dini, ndivyo ubabedume unavyozidi kuimarika.

**2:5 Asasi ya Elimu**

Elimu ni muhimu sana katika maisha ya binadamu. Hata hivyo mfumo wa ubabedume haumpi mwanamke nafasi ya kupata elimu. Tujuavyo ni kwamba manufaa ya elimu ni mengi. Hivyo basi mwanamke anapitwa na mambo mengi kwa kukosa elimu. Millet (k.h.j:42) anasema, "Kama elimu ni nguvu, nguvu pia ni elimu. Sababu kuu ya kufaulu kwa mfumo wa ubabedume ni kuwa unamnyima mwanamke elimu." Hata pale mwanamke anapopata elimu, elimu hiyo ni duni ikilinganishwa na ile ya mwanamume. Bell na Offen (k.h.j:47) wanasema kuwa mwanamke hapaswi kupewa elimu sawa na mwanamume.

Mwanamume anapaswa kupewa elimu ya juu zaidi. Kupitia kwa elimu, binadamu amejifunza mambo mengi na kuvumbua mengi hasa katika sayansi na teknolojia.

Hapo zamani binadamu alikumbwa na majanga mengi kama vile ukame, mafuriko na magonjwa yasiokuwa na tiba. Baada ya kuelimika na kufanya utafiti, aliweza kusuluhisha baadhi ya matatizo hayo. Alitengeneza dawa, kunyunyizia mimea maji, na kuhifadhi chakula vizuri ili kimfae wakati wa ukame. Ufanisi huu uliweza kufikiwa kwa kuwa alielewa mazingira yake na kuyatumia ili yamfae. Mambo haya yalifanywa na wanaume. Kwa upande mwingine, mwanamke alidhibitiwa na mfumo wa ubabedume na kutoshirikishwa katika maendeleo haya. Mwanamke alibaki nyumbani na kunyimwa nafasi ya kupata elimu. Hadhi ya mwanamke ikazidi kudhoofika zaidi katika jamii. De Beauvoir (k.h.j:135) anasema, "Mwanamke aliishi maisha ya kumtegemea mwanamume. Hakupata elimu muhimu na hakuweza kushiriki kikamilifu katika maendeleo." Maoni haya yanaungwa mkono na Gerda (k.h.j:223) anayesema, "Wanawake walinyimwa haki ya kupata elimu na hivyo basi wakaachwa nje katika historia.

Kumnyimwa mwanamke elimu ndiko kumechangia zaidi nafasi duni ambayo amepewa katika jamii. Madai haya yana ukweli mwingi. Wanawake walioelimika huweza kutambua haki zao na kuzidai ilhali baadhi ya wanawake ambao hawakufanikiwa kupata elimu hushindwa kutambua haki hizo.

### 2:6 Hitimisho

Katika sura hii, tumeshughulikia ubabedume kama mhimili mkuu wa upembezwaji wa mwanamke. Tumeeleza historia ya ubabedume kwa sababu uelewa wetu wa historia hii,

utatusaidia kuelewa namna upembezwaji wa mwanamke unavyojitokeza katika *Utenzi wa Fatuma.*

Aidha tumeonyesha kuwa asasi za ndoa, dini, utamaduni na elimu ndizo zinazochangia kuendeleza mfumo wa ubabedume. Mfumo huu umeshughulikiwa katika sura hii kwa sababu unatupa msingi wa kuhakiki swala la upembezwaji wa mwanamke katika *Utenzi wa Fatuma.*

Katika sura ya tatu, tutauhakiki *Utenzi wa Fatuma* kwa kutumia nadharia ya ufeministi wa kirasimi. Uhakiki wetu utazingatia asasi zinazochangia upembezwaji wa mwanamke.

# SURA YA TATU

## UHAKIKI WA *UTENZI WA FATUMA*

### 3:0 Utangulizi

Katika sura ya pili tumeshughulikia ubabedume kama mhimili mkuu wa upembezwaji wa mwanamke.

Katika sura hii ya tatu,tutauhakiki *Utenzi wa Fatuma* kwa kutumia nadharia ya ufeministi wa kirasimi. Uhakiki huu utazingatia asasi zinazochangia upembezwaji wa mwanamke. Asasi hizi ni: ndoa, dini na utamaduni. Hatutashughulikia asasi ya elimu kwa kuwa haijitokezi katika utenzi huu. Kwa kuwa ni vigumu kuweka mipaka dhahiri kati ya dini, ndoa na utamaduni, tutazishughulikia asasi hizi kwa pamoja.

### 3:1 Upembezwaji wa mwanamke katika *Utenzi wa Fatuma*

Mwanamke amepembezwa kwa njia mbalimbali katika *Utenzi wa Fatuma.* Katika sehemu hii tutadhihirisha namna upembezwaji wa mwanamke unavyojitokeza kupitia asasi tulizozitaja hapo juu.

#### 3:1:1 Maisha ya Fatuma Kabla ya kuolewa

Fatuma alizaliwa na kukulia katika mazingira yaliyoathiriwa kwa kiasi kikubwa na dini ya Kiislamu. Kwa kuwa babake Fatuma ndiye aliyekuwa mwanzilishi wa dini ya Kiislamu, ilimbidi Fatuma ayafuate na kuyazingatia mafundisho ya dini hii.

Kabla ya kuolewa, Fatuma alikaa nyumbani na kujishughulisha na shughuli za nyumbani kama tunavyoona katika ubeti huu:

Endapao msikitini, kisa kusali Amini,

Arudiapo nyumbani, ali kimlingania (ubt 98).

Kulingana na ubeti huu, mwanamke amepembezwa kwa kutoshirikishwa katika shughuli zinazofanyika nje ya nyumba.

Fatuma analazimika kukaa nyumbani kwa kuwa dini ya kiislamu haiwaruhusu wanawake kutangamana na wanaume ovyo. Maududi anasema:

> Lengo la dini ya Kiislamu ni kuibua mfumo wa kijamii ambao unatenganisha mahusiano ya wanaume na wanawake na kuhakikisha kuwa hakuna maingiliano ya kijinsia yanayoweza kuhatarisha nidhamu ya kimaadili katika jamii....uhuru wenye mipaka na masharti ambao mwanamke alikuwa amepewa na dini ya Kiislamu katika maswala ambayo hayahusiani na sayansi ya nyumba, unatumiwa kama tetesi ya kuwahimiza wanawake Waislamu kuasi maisha ya nyumbani na wajibu wake. Wanafanya hivi kwa kuwaiga wanawake wazungu. Tetesi kama hizi zitawafanya wanawake Waislamu kuishi maisha ya upweke huku wakinga'anga'ania shughuli za kisiasa, kijamii na kiuchumi bega kwa bega na wanaume. (1974:21)

Hivyo basi, Fatuma analazimika kukaa nyumbani ilhali babake na wanaume wengine wanatoka na kwenda mahali popote wapendapo kwa shughuli mbalimbali. Kwa hivyo, mwanamke analazimika kukaa kando na kutazama huku mwanamume akiendelea na shughuli muhimu huko nje. Mwanamke amepembezwa katika utenzi huu.

**3:1:2 Kuposwa kwa Fatuma**

Baada ya kifo cha Khadja, Mtume Muhammad alifikiria sana kuhusu mwanawe Fatuma. Alitaka Fatuma aolewe:

Fikira zakwe Tume, alikimwaza mume;
Alo mwema, amwengeme, mwenye kumkhutubia (ubt 107).

Alipofikiwa wakati, wa kubalighi binti,
Alizidi wema siti, na nuru kumzagaa. (ubt 108)

Hapo kazidi Rasuli, hamu khuu na shughuli
Kwa mtana na leili, kula wakati na mia (ubt 109)

Kitamani moyowe, kumtambua mkwewe.
Na kungojeza ambiwe, na risala Jiburia (ubt 110).

Swala la kuolewa kwa Fatuma linamsumbua sana Mtume Muhammad. Hii ni kwa kuwa katika dini ya Kiislamu, ni jukumu la wazazi kuwatafutia wasichana wao wanaume wa

kuwaoa. Katika dini ya Kiislamu, ndoa ni asasi ya lazima. Hii ni sababu nyingine ambayo ilimfanya Mtume Muhammad kuwa na taharuki kuhusiana na ndoa ya mwanawe Fatuma. Labda alihisi kuwa alikuwa na kibarua kigumu cha kumtafutia bintiye mume kwa kuwa bibi yake hakuwepo tena kumsaidia kufanya kazi hii. Mtume aling'ang'ana kutimiza wajibu wake kama mzazi kulingana na dini ya Kiislamu. Iqbal anasema:

> Kulingana na mtazamo wa dini ya kiislamu, ndoa ni asasi ya lazima na isipokuwepo, maisha ya binadamu hayawezi kusemekana kuwa yamekamilika hapa duniani. Katika dini ya kiislamu, ndoa ni namna ya kuabudu na humwezesha mtu kumkaribia Mungu. (1989:15)

Maoni haya yanaungwa mkono na Abd-al-Afi (1977:52) anayesema kuwa ndoa ni asasi ya lazima katika dini ya Kiislamu. Katika *Utenzi wa Fatuma*, Mtume Muhammad peke yake ndiye anayeonekana kushughulikia ndoa ya Fatuma. Fatuma hausiki. Jambo hili linadhihirika vizuri zaidi wakati watu kadhaa walipokuja kumposa Fatuma. Posa hizo hazipelekwi kwa Fatuma bali kwa babake:

> Kwa wothe masultani, mitima ikitamani:
> "Nenda mimi kwa Amini, kumposa Jauharia!" (ubt 121)

> Islamu na kufari, kula mthu kazamiri:
> "Nenda mimi kwa Bashiri, kukhutubu Shamsia." (ubt 122)

Katika shughuli hii ya posa, Fatuma amepembezwa kwa kiasi kikubwa. Amebaki kuwa mtazamaji katika shughuli muhimu inayomhusu. Babake ndiye anayefanya maamuzi yote.

Mwanamke hajashirikishwa katika kufanya maamuzi muhimu yanayomhusu. Uamuzi kuhusu ni nani atakayemwoa mwanamke fulani, unapaswa kuwachiwa mwanamke husika. Mwanamke amepembezwa katika *Utenzi wa Fatuma* kwa kutoshirikishwa katika maamuzi yanayohusu maisha yake.

### 3:1:3 Ndoa ya Fatuma Mbinguni

Ndoa katika dini ya Kiislamu huwa na hatua mbili. Marzouqi (2000:192), anasema kuwa ndoa katika dini ya Kiislamu huwa na hatua mbili: posa, na ndoa yenyewe. Katika *Utenzi wa Fatuma*, watu wengi walituma posa zao kwa Mtume Muhammad wakitaka kumwoa Fatuma. Baadhi ya watu hao walikuwa matajiri na watu maarufu:

> Kwa wothe Masultani, mitima ikitamani:
> "Nenda mimi kwa Amini, kuposa Jauharia!" (ubt 121)
>
> Wakazandika nyaraka, kula mthu kupeka
> Za kuposa na kutaka, mwanamke kumuowa (ubt 123)

Baadhi ya watu waliotuma posa zao, walikuwa makafiri. Makafiri hawa walijifanya kuwa wamesilimu kwa imani kuwa wakifanya hivyo, posa zao zitakubaliwa na Mtume Muhammad. Hata hivyo, juhudi zao hazikuwafaa kitu:

> Masultani kufari, kusilimu wakakiri,
> Kwa ndowa yakwa zahari, ambayo akubalia (ubt 123)

Kasilimu nafusiye, pamoja na kaumuye,
Mtumi asirizie, jawabu kuwajibia (ubt 129)

Kula endao kutaka, asijibu Nabiyaka.
Neno lema la kushika, au la kuwakataa (ubt 130)

Makafiri walilazimika kujifanya kuwa wamesilimu kwa sababu katika dini ya Kiislamu, mwanamke hawezi kuolewa na mwanamume ambaye si Mwislamu. Al-Marzouqi anasema:

> Mwanamke Mwislamu hakubaliwi kuolewa na mwanamume ambaye si Mwislamu kwa kuwa sheria za dini ya Kiislamu haziwezi kutumika kwa mtu ambaye si Mwislamu. Iwapo mwanamke Mwislamu ataolewa na manamume ambaye si Mwislamu, itakuwa vigumu kutatua matatizo yao ya kindoa kwani sheria za Kiislamu hazitaweza kutumika. (2000:191)

Kama tulivyoeleza katika sura ya pili dini inaendeleza ubabedume. Matajiri na makafiri hao waliosilimu hawakufanikiwa kumwoa Fatuma. Mtume Muhammad alingoja ishara kutoka kwa Mwezi Mungu kupitia kwa malaika Jibrili.

Kitamani moyowe, kumtambua mkwewe,
Na kungojeza ambiwe, na risala Jiburia. (ubt 110)

Ali alitamani sana kumwoa Fatuma lakini hakumposa kwa kuwa hakuwa na mali ya kulipa mahari. Ali aliweka imani yake kwa Mungu na kuomba.

Kitamani kwa kweli, kumwowaye batuli,

Alikihofu makali, kunena na Mursa. (ubt 146)

Kuikosakwe kwa kithu, kikiwafi penye wathu,

Moyowe kafanya phitu, asipende kutongoa (ubt 148)

Hata ingawa Ali hakuwa na mahari kwa sababu ya umaskini wake, hatimaye alifanikiwa kumwoa Fatuma. Ndoa kati ya Fatuma na Ali inafanyika mbinguni baada ya Mungu kuyajibu maombi ya Ali. Huko duniani, Fatuma hana habari yoyote kuwa Ali atakuwa mumewe. Posa ya Ali inakubaliwa na kuidhinishwa na Mwenyezi Mungu mbinguni kwa kuwa Waislamu wanaamini kuwa, kati ya sababu kadha zinazowafanya watu kuoa, sababu kuu na muhimu kabisa ni unyenyekevu na utiifu wa Mungu. Imran anasema:

> Mwanamke anapoteua mwanamume wa kuolewa naye, jambo la kusisitizwa ni utiifu na unyenyekevu kwa Mungu na wala sio utajiri. Iwapo mtu ana majaliwa ya kuwa tajiri, atakuwa tajiri hatimaye. Wasichana wengi walioolewa na maskini wameishia kuishi maisha ya raha na starehe. Kwa upande mwingine, wasichana walioolewa na matajiri na wafalme wameishia katika maisha ya upweke. (1981:11)

Katika ndoa inayofanyika mbinguni, Mungu alimwakilisha Fatuma, malaika Jibrili akamwakilisha Ali naye malaika Mikaili akawa shehe:

Akimuoza Alia, bum amuyo, Nabia,

Na rabi ndiye walia, fahamu, ewe nabia! (ubt 274)

Nami ndimi nimkubali, wa kumwolea Ali,

Na ndu yangu Mikaili, ndiye alokhutubia (ubt 275)

Fatuma anawakilishwa na Mungu. Mwanamke amepembezwa kwa kuwa anawakilishwa na mwanamume na wala sio mwanamke mwenzake. Matarajio yetu ni kuwa, mwanamke anapaswa kuwa mtu wa kwanza kuhusishwa katika ndoa yake. Ndiye anayeolewa. Itakuwaje mtu anayeolewa akose kwenye sherehe ya kumwoza? Katika dini ya Kiislamu, mwanamke hana lazima ya kuwepo katika sherehe za ndoa yake. Wanaume peke yao wanatosha kuendesha sherehe hiyo. Mwanamke anaweza kuwakilishwa na mwanamume kama baba, babu au ndugu wa karibu katika familia.

Al-Marzouqi (2000:196) anasema, "Kulingana na hadithi za Mtume Muhammad, kunapaswa kuwa na msimamizi au mwakilishi wa mwanamke wakati wa kufunga ndoa." Naye Seif-Al-Hatimy anasema:

Usimamizi ni jukumu la baba au ndugu wa kiume aliyekaribu kabisa kiukoo katika familia, kuwasimamia watu ambao hawana akili timamu, watoto au wale wasiokuwa na tajiriba katika maswala fulani. (1979:70).

Fatuma kama kielelezo cha mwanamke katika utenzi huu anadhihirisha picha ya mwanamke aliyegandamizwa. Ni kana kwamba mwanamke hana umuhimu wowote. Kuwepo au

kutokuwepo katika sherehe ya ndoa yake hakuna umuhimu wowote. Hii ni dhihirisho wazi kuwa dini inachangia pakubwa kuimarika kwa mfumo wa ubabedume.

**3:1:4 Ndoa ya Fatuma duniani**

Malaika Jibrili anatumwa na Mungu duniani kumjulisha Mtume Muhammad kuhusu ndoa iliyofanyika mbinguni kati ya bintiye Fatuma na Ali:

> Wakisa kusikilia, Jiburili kamwambia,
> Kaketi kalingania, makaoni akakaa. (ubt 262)

> Hapo alipolingana, mbee zake Nabiina,
> Kamwambia, "Subhana, akusalimu, Nabia!" (ubt 263)

> Akamba: "ewe Rasuli meozwa mwano batuli,
> Na mume ni Shekhe Ali, ndiye mume Alia." (ubt 273)

Matarajio yetu ni kuwa malaika Jibrili angepeleka habari hizi moja kwa moja kwa Fatuma. Lakini sivyo, malaika Jibrili anapeleka habari hizo kwa Mtume Muhammad. Fatuma anajulishwa kuhusu ndoa kati yake na Ali baadaye. Wakati Mtume anamjulisha bintiye kuhusu ndoa hii, uamuzi ulikuwa tayari umefikiwa na wanaume peke yao na Fatuma anakuwa mtu wa mwisho kupata habari kuhusu ndoa yake. Mwanamke amepembezwa kiasi cha kauli yake kutohitajika katika mambo yanayomhusu. Fatuma anapopashwa habari hizi anakubali kuolewa. Hana lingine la kufanya. Kukataa kuna maana kuwa anapinga mafundisho ya dini ya Kiislamu. Iwapo mwanawe Mtume Muhammad atapinga mafundisho

ya dini ya Kiislamu, nani atakayeyakubali mafundisho hayo? Kwa hivyo dini ya Kiislamu imempembeza mwanamke katika *Utenzi wa Fatuma.*

### 3:1:5 Mahari

Mahari ni muhimu sana katika ndoa, kulingana na dini ya Kiislamu ndoa huwa haijakamilika ikiwa mahari hayakulipwa. Zeba (1976:38) anasema, "hakuna ndoa ambayo inaweza kukamilika bila ya mwanamume kulipa mahari kwa mwanamke anayemwoa." Hii ni kwa kuwa sababu kuu ya kulipwa kwa mahari ni kudhihirisha uwezo wa mwanamume wa kumtunza mkewe. Al-Marzouqi (2000:203) anasema, "Mahari hulipwa kama hakikisho kutoka kwa mwanamume kuwa ana uwezo wa kumtunza mkewe." Mahari hulipwa na mwanamume au familia yake kwa msichana au familia yake. Seif-Al-Hatimy (k.h.j:62) anasema, "Mahari yanapaswa kulipwa na mwanamume au familia ya mwamume kwa mwanamke au familia ya mwanamke. Mahari yanaweza kuwa pesa, madini au vitu vingine vya thamani." Kutokana na fafanuzi hizi, ni wazi kuwa mahari ni muhimu sana katika ndoa.

Katika *Utenzi wa Fatuma,* Ali hakuwa na uwezo wa kumlipia Fatuma mahari. Baada ya ndoa yao kufungwa mbinguni, Mungu anawatuma malaika duniani kupeleka mahari kwa Fatuma:

> "Ewe, malaika wangu, tukuwa risala yangu,
> Wende kwa Mtume wangu, sasa katika dunia (ubt 241)
>
> Sikia wewe yakini, na nduguzo wa mbinguni
> Wathu zikwi sab'ini, wenye kukufuwatia! (ubt 242)

Na wothe watweke mali, tabaki nyingi sakili,

Kwa kula mthu himli, awezao kutukua (ubt 246)

Mahari ni mahitaji ya ndoa ambayo yanachangia pakubwa kupembezwa kwa mwanamke. Mwanamke hahusishwi katika kutoa maamuzi kuhusiana na swala la mahari. Mwanamke amepembezwa kwa kutohuzishwa katika kuamua kiasi cha mahari kitakachotolewa. Katika utenzi huu, Fatuma analetewa mahari kutoka mbinguni. Hata kama hayakubali mahari hayo, ni wazi kuwa hakukuwa na nia ya kumhusisha katika swala hili. Baada ya arusi kufanyika mbinguni, mahari yanatolewa moja kwa moja na kupewa malaika elfu sabini wampelekee Fatuma:

Ewe, malaika wangu tukuwa risala yangu,

Wende kwa Mtume wangu, sasa katika dunia! (ubt 241)

Sikilia wewe yakini, na nduguzo wa mbinguni ,

Wathu zikwi sab'ini, wenye kukufuatia! (ubt 242)

**3:1:6 Mwanamke na Ubikira**

Fatuma amelinganishwa na bikira wa mbinguni. Hawa ni viumbe ambao kulingana na dini ya Kiislamu wanaaminiwa kuwa wanaishi mbinguni na ni watakatifu. Wema wa Fatuma unasemekana kuwa umepita ule wa bikira hawa wa mbinguni:

Mwana wa Thumwa Amini, hoyo mamaye Hasani,

Haiwi khurulaini, kumfa`nidia. (ubt 94)

Khurulaini phambie, hawapati shabihihi,

Launi na tabi`aye, hakuoneka misaa. (ubt 95)

Alikiwapita khuri, kwa mambo mangi kasiri;

Sifa zakwe na kadiri, haku kamaye asia. (ubt 96)

Beti hizi zinathibitisha kuwa Fatuma alikuwa bikira kabla ya kuolewa. Mfumo wa kiubabedume unachangia kupembezwa kwa mwanamke kwa kuwataka kuwa bikira kabla ya kuolewa. Millet anasema:

Mfumo wa kibabedume uhimiza kuwa wanawake wawe bikira kabla ya kuolewa. Ubikira huwa thibitisho kwa mwanamume anayeoa kuwa amepokea 'mali' ambayo hayajatumia na mtu mwingine. (k.h.j :42) Waislamu wanaamini kuwa bikira hawa watakatifu huishi maisha mazuri huko mbinguni. Kwa sababu hii, ubikira unahimizwa sana kwa wasichana Waisilamu. Kutokuwa bikira kabla ya kuolewa kuna maana kuwa msichana alishiliki kitendo cha kufanya mapenzi. Kitendo hiki hutendwa na watu wawili; mwanamume na mwanamke. Kwa nini basi mwanamke awe ndiye wa kulaumiwa kwa kutokuwa bikira? Kwa nini mwanamume vilevile hakutakiwa kuwa bikira kabla ya kuoa? Kumtaka mwanamke kuwa

bikira wakati wa ndoa na kutomtaka mwanamume kuyatii masharti hayo hayo, ni kumpembeza. Katika sura ya pili, tuliona kuwa mwanamume alipomiliki ardhi, alitaka pia kummiliki mkewe na watoto ili wamfanyie kazi shambani. Mwanamume huyu alitaka kuwamiliki watoto pia kwa sababu alitaka warithi ardhi hiyo atakapoaga dunia. Mwanamume huyu hakutaka ardhi yake irithiwe na watu ambao hawakuwa wa ukoo wake. Hii ndio sababu iliyompelekea kutaka kuwa mtu wa pekee mwenye mahusiano ya kimapenzi na mkewe. Hali hii ndio iliyosababisha mahitaji ya mwanamke kuwa bikira kabla ya kuolewa. Kutokana na haya, ni wazi kuwa mahitaji ya mwanamke kuwa bikira yalianzishwa na wanaume ambao walikusudia kuendeleza mfumo wa ubabedume. Katika utenzi huu, Fatuma anasifiwa sana kwa kuwa bikira:

Wema wa Mwana batuli, binti Thumwa Rasuli,
Ukenea filhali, shariki na gharibia. (ubt 111)

Kitamani kwa kweli, kumwowaye batuli,
Alikihofu makali, kunena na Mursaa. (ubt 146)

Mwenye Ezi, Mfazali, akamba ndiyo ni kweli,
Ndoa ndakwe batuli, mwanamke mfazaa. (ubt 227)

Ubikira ni sifa inayomfanya Fatuma awavutie wanaume wengi. Sifa hii ya ubikira inasaidia kumsawiri mwanamke kama kiumbe aliyepembezwa (yaani kiumbe aliyehifadhiwa vyema, ametunza na kuhifadhiwa mahali fulani katika jamii ili asitangamane na ulimwengu unaoweza kumharibu).

**3:1:7 Mwanamke kama mzazi na mlezi.**

Mwanamke katika *Utenzi wa Fatuma* amesawiriwa kama mzazi na mlezi. Khadja, mkewe wa kwanza wa mtume Muhammad, ameelezwa kuwa mzazi wa Hassani na Husseini. Khadja ameelezwa pia kuwa mlezi wa watoto wake:

Mwana wa Thumwa Amini, hoyo mamaye Hassani,
Haiwi khurulaini, kamwe kumfanidia. (ubt 94)

Mtume wethu Amini, kangia khuu huzuni,
Kuondoka mke shani, mwenye kuyea sabia. (ubt 103)

Mlezi wa wakwe wana, kwa kuwata kumuona,
Kwa usiku na mtana, mtume halikituwa. (ubt 104)

Kwa laza zakwe hakika, kwa zothe zalipunguka,

Kwa Khadja kutoweka, kuwa Muyezi Nabia. (ubt 105)

Mwanamke ni mzazi na mlezi katika jamii hii. Haikosi kuwa Fatuma alipata umaarufu wake kwa kuwa ndiye mama yao Hassan na Hussein.Wajibu wa mwanamke kama mzazi unatambulikana sana. Mtume Muhammad anaathirika vibaya baada ya kifo cha mkewe Khadja. Ajabu ni kwamba, baadala ya mtume kuathirika kwa kupoteza mpenziwe na mwenziwe, anaathirika kwa sababu baada ya kifo cha Khadja, hakukuwa na mtu wa kutekeleza wajibu uliokuwa ukitekelezwa na mkewe. Mtume anasononeka kwa kuwa hakuwa na mke wa pili:

Mwana Khadja kufake, Mtume kaka pweke;

Asina wa pili wake, Mtume akatoshea. (ubt 102)

Mwana Khadja kufake, Mtume kaka pweke;

Asina wa pili wake, Mtume akatoshea. (ubt 102)

Kutokana na ubeti huu tunajipata tukijiuliza swali; je, kama mtume angelikuwa na mke wa pili, angeomboleza? Hii ni kwa kuwa ubeti huu unatueleza wazi kuwa mtume aliathirika vibaya kwa kuwa hakuwa na mke wa pili. Mwanamke katika utenzi huu amepembezwa kwa kuwachiwa jukumu ngumu la kuwalea watoto peke yake. Mwanamume hashiriki katika kazi hii ngumu ya malezi hata ingawa yeye ni mzazi kama alivyo mwanamke. Ni maoni ya mtafiti huyu kuwa Mtume Muhammad alijuta kwa kutokuwa na mke wa pili Khadja alipofariki. Hii

ni kwa kuwa jambo ambalo limesisitizwa ni majukumu ya malezi yaliyokuwa yakitekelezwa na Khadja. Mtume Muhammad anatatizwa na swala la malezi ya wanawe. Mwanamume hataki kushiriki katika ulezi wa watoto. Jukumu hilo linatengewa wanawake.

Mwanamke amesawiriwa kama mlezi. Mtume anasemekana kuwa alihuzunika sio tu kwa kumpoteza mkewe bali pia kwa kupoteza mama aliyelea watoto wake. Tunaelezwa kuwa mtume hakuwa na amani kwa kumpoteza mama aliyewalea watoto wake. Alihuzunika kwa kuwa hangeweza tena kumuona mchana na usiku. Jambo hili linaingiliana na mafundisho ya dini ya Kiislamu kuwa sababu kuu ya ndoa ni kuzaa na kuwalea watoto ili kuendeleza kizazi. Seif-Al- Hatimy (1979:54) anasema kuwa sababu kuu ya ndoa katika dini ya Kiislamu ni kuzaa watoto. Mwanamke ndiye aliyepewa jukumu la kulea watoto na wala si mwanamume. Hii ndio sababu mtume alihuzunika zaidi. Jambo hili limehimizwa katika ubeti wa mia moja na kumi na tano ambapo tumeelezwa kuwa raha zake zote zilipunguka na mtume akalazimika kuwalea watoto wake mwenyewe. Kwa hivyo, mwanamke humfanya mwanamume kuona raha maishani na vilevile amepewa jukumu muhimu la kuwalea watoto. Kutokana na ubeti huu, ni dhahiri kuwa kazi ya kulea watoto haina raha yoyote. Pili, mwanamume huiepuka kazi hii muhimu isiyokuwa na raha yoyote na kumwachia mwanamke kuifanya. Basi, ni wazi kuwa mwanamke amegandamizwa. Kwa nini ametengewa kazi ngumu ya kuwalea watoto? Ni kwa nini kazi hii inasemekana kuwa haina raha? Haya ni maswali ambayo bila shaka majibu yake yatatupelekea kwenye hitimisho kuwa mwanamke amepembezwa kwa kuwachiwa jukumu ngumu la kuwalea watoto.

## 3:2 Hitimisho

Katika sura hii, tumeukakiki *Utenzi wa Fatuma* kwa kutumia nadharia ya ufeministi wa kirasimi. Nadharia hii imethibitisha kuwa asasi za ndoa, dini na utamaduni zinachangia kupembezwa kwa mwanamke katika *Utenzi wa Fatuma.* Kwa mfano, Fatuma hahuzishwi katika shughuli za kumposa, katika mipango ya ndoa yake, katika sherehe ya ndoa hiyo wala katika shughuli za uzalishaji mali.

Katika sura inayofuata, tutashughulikia matumizi ya lugha na kuonyesha jinsi yanavyochangia kujenga maudhui ya upembezwaji.

# SURA YA NNE

## MATUMIZI YA LUGHA KATIKA *UTENZI WA FATUMA* .

### 4:0 Utangulizi

Katika sura ya tatu tumeuhakiki *Utenzi wa Fatuma* kwa kuzingatia asasi zinazochangia katika upembezwaji wa mwanamke.

Katika sura hii ya nne, tutachunguza namna matumizi ya lugha yanavyochangia kujenga maudhui ya upembezwaji wa mwanamke katika *Utenzi wa Fatuma.* Mbinu ambazo zimetumiwa kumpembeza mwanamke kwa mapana ni ishara na uashiriaji na vilevile Sitiari.

### 4:1 Ishara na uashiriaji

Katika utenzi huu tumeelezwa kuwa Mungu aliumba milima, wanyama, malaika na kadhalika. Baada ya kuumba, Mungu alichagua vitu au viumbe wanne ambao aliwaona kuwa bora zaidi. Katika kuorodhesha vitu na viumbe hawa, mwanamke anatajwa akiwa wa mwisho. Orodha ilioyotumika katika ufafanuzi huu ni kama ifuatayo: malaika, vitabu, watume, watu, milima, miezi, siku, usiku na wanawake. Katika orodha hii wanaume kama malaika na mitume wanatanguliwa kutajwa. Je, ni kwa nini mwanamke hatangulii kutajwa katika orodha hii?

Tungetarajia kuwa mwanamke angeorodheshwa pamoja na watu wengine (wanaume), lakini sivyo kabisa; mwanamke ameorodheshwa baada ya milima, siku, miezi na vitabu. Orodha hii ni ishara inayoashiria upembezwaji wa mwanamke katika utenzi huu. Kwa nini akawa wa mwisho kutajwa? Hata ingawa hatujui ni kigezo gani kulichotumiwa katika kuorodhesha

huku, ni maoni yetu kuwa mwanamke amepembezwa kwa kuelezwa mwisho kabisa baada ya viumbe visivyokuwa na uhai. Aidha, tunaweza kujiuliza, ni kwa nini malaika, vitabu vitakatifu na mitume wakaelezwa kwanza? Haikosi kuwa swala la hadhi lilizingatiwa katika maelezo hayo. Kwa hivyo, mwanamke amepembezwa na kuchukuliwa kama kiumbe wa hadhi ya chini akilinganishwa na viumbe wengine walioumbwa na Mungu. Isitoshe, utenzi huu unamhusu Fatuma ambaye ni mmoja kati ya wale wanaotajwa katika orodha hii ya mwisho. Kwa nini hakutangulia kuelezwa? Kupembezwa huku kwa mwanamke katika utenzi huu, ndiko kunakomfanya adhulumiwe na kupewa hadhi ya chini kabisa. Ni maoni yetu kuwa Kama mwanamke hapembezwi, basi hangeliorodheshwa pamoja na wanaume.

### 4:2 Sitiari

*Sitiari ni mbinu ya ulinganishi* ambayo haijitokezi moja kwa moja kama tashbihi.Baadhi ya sitiari ambazo mtunzi ametumia ni:

#### 4:2:1 Fatuma kama chombo

Katika Utenzi wa Fatuma, Mwanamke amesawiriwa kama chombo cha kumvutia na kumfurahisha mwanamume. Urembo wake umefananishwa na mwezi. Kwa hivyo, kama mwezi ung`aapo na kuvutia hasa usiku, ndivyo mwanamke anavyong`aa na kuvutia. Mwanamke anapolinganishwa na mwezi anakuwa kama chombo cha kumvutia na kumridhisha mwanamume. Mwanamke ni kiumbe muhimu sana katika jamii kwani ndiye anayeweshesha kuwepo na kuendelea kuwepo kwa kizazi cha binadamu duniani. Si haki kumfananisha kiumbe huyu na vitu kama vile mwezi. Suala la mwanamke kuchukuliwa kuwa

kama kiumbe anayemfurahisha mwanamume limetiliwa nguvu na madai kutoka kwa utenzi huu kuwa, anayemtazama hutosheka.

Ila hoyo Fatuma, ali azidie wema,

Na jamala ya daima, isiyomtindika. (Ubt 91)

Usowe walina nuru, aziada *l-kamaru;*

Mwenye kumtanazaru, mthu alikitoshea.  Ubt (92)

Ali aumbiwe sana, kwa mae yakwe na pana;

Haku mwenye kumuona, kaweza kumwangalia.  Ubt (93)

Urefu wa mwanamke umeelezwa kuwa wa kuvutia. Vivyo hivyo, upana wake unasemekana kuwa hauna mfanowe. Umbile lake limeelezwa kuwa la kupendeza sana. Urembo wake unazidi kusisitizwa hadi kufikia kiwango kuwa mwanamke huyu anafananishwa na maua na vilevile matunda:

Hapo kuondoka Rasuwa, kalendea lake uwa;

Yothe aliyoambiwa, nae kenda kamwambia:   ubt (284)

"Ewe, tunda la moyowa, Fatuma mwenye muruwa,

Uniilie Rasuwa, ma`alimu Jiburia. Ubt (285)

Maelezo haya yanatuchorea picha ya kiumbe ambaye ni kifaa au chombo cha urembo. Mtu anapoona maua mazuri, anayachuna na kuyaweka ndani ya nyumba yake ili azidishe haiba ya nyumba hiyo. Kumfananisha mwanamke na maua haya kunamdhalilisha na kumshushia hadhi yake kama binadamu. Mwanamke katika *Utenzi wa Fatuma* amesawiriwa kama chombo cha kunadiwa sokoni. Uzuri na urembo wa Fatuma ulienea kote ulimwenguni: Arabia, Misiri, Uropa na kadhalika:

Dili hata Ulaya, Khabari zikaenea,

Pasisalie pamoya, mwezi usipoenea. (ubt 115)

Ulimwengu wothe pia, sifa zakwe zikanea,

Pasisalie pamoya, wathu wasiposikia. (ubt 119)

Mwanamke amechukuliwa kuwa kivutio kwa wanaume. Urembo wake unaelezwa kwa njia nyingi. Hatuoni wakati wowote ambapo anasawiriwa au kuelezwa kuwa mwenye bidii au kupewa sifa ingine yoyote muhimu; urembo wake tu ndio unaosisitizwa. Kwa hivyo, mwanamke amesawiriwa kama chombo kinachopendeza na ambacho kipo tayari kununuliwa na mtu yeyote yule. Inabainika kuwa umuhimu wa mwanamke unaonekana tu katika urembo

wake. Urembo huu umehimizwa kiasi kwamba mwanamke anaonekana kuwa kiumbe ambaye hawezi kujikimu wala kujisaidia kwa lolote lile; urembo wake pekee ndio muhimu katika maisha yake. Ni chombo cha thamani kama dhahabu au almasi ambayo kila mwanamume anataka kuinunua ili iwe pambo nyumbani kwake. Jambo hili linahimizwa zaidi kutokana na sifa alizopewa fatuma na baadhi ya wanaume waliokuja kumposa. Walimpa majina kama jua na madini; vitu vinavyong`aa na kupendeza:

> Kwa wothe masultani, mitima ikitamani:
>
> "Nenda mimi kwa Amini, kuposa Jauharia! " (ubt 121)

Neno jauharia lina maana ya madini. Kwa hivyo, anayesema maneno haya, anataka kumposa kiumbe huyu anayemfananisha na madini; kitu kinachovutia. Labda hata kama mwananamke huyu angelikuwa na sifa na tabia nzuri kiasi gani, mwanamume huyu hangelimposa kwa kuwa hang`ai kama madini:

> Islamu na kufari, kula mnthu kuzamiri:
>
> "Nenda mimi kwa Bashiri, kukhutubu shamsia!" (ubt 122)

Neno shamsia lina maana ya jua. Kwa hivyo, mwanamume huyu anataka kumposa msichana anayemetameta kama jua. Amevutiwa na mwanamke huyu jinsi nondo anavyovutiwa na taa usiku. Kwa jumla, taswira tunayoipata ni ya wanaume kutoka kila pembe ya dunia wakipigania kumposa Fatuma. Kila mmoja anatuma maombi yake kuposa "jua", "madini", na

"nyota". Mwanamke amedunishwa kiasi cha kuonekana kuwa chombo au madini adimu, ndiposa kila mtu anapigania kukipata.

### 4.2.2 Fatuma kama Khurulaini

Fatuma amelinganishwa na bikira wa mbinguni au Khurulaini. Hawa ni viumbe ambao kulingana na dini ya Kiislamu wanaaminiwa kuwa wanaishi mbinguni na ni watakatifu. Wema wa Fatuma unasemekana kuwa umepita ule wa bikira hawa wa mbinguni:

Mwana wa Thumwa Amini, hoyo mamaye Hasani,
Haiwi khurulaini, kumfa`nidia. (ubt 94)

Khurulaini phambie, hawapati shabihihi,
Launi na tabi`aye, hakuoneka misaa. (ubt 95)

Alikiwapita khuri, kwa mambo mangi kasiri;
Sifa zakwe na kadiri, haku kamaye asia. (ubt 96)

Waislamu wanaamini kuwa bikira hawa watakatifu huishi maisha mazuri huko mbinguni. Kwa sababu hii, ubikira unahimizwa sana kwa wasichana Waislamu. Kutokuwa bikira kabla ya kuolewa kuna maana kuwa msichana alishiriki kitendo cha kufanya mapenzi. Kitendo hiki

hutendwa na watu wawili; mwanamume na mwanamke. Kwa nini basi mwanamke awe ndiye wa kulaumiwa kwa kutokuwa bikira? Kwa nini mwanamume vilevile hakutakiwa kuwa bikira kabla ya kuoa? Kumtaka mwanamke kuwa bikira wakati wa ndoa na kutomtaka mwanamume kuyatii masharti hayo hayo, ni kumgandamiza na kumdunisha mwanamke.

Katika sura ya pili, tuliona kuwa mwanamume alipomiliki ardhi, alitaka pia kumiliki mkewe na watoto ili wamfanyie kazi shambani. Mwanamume huyu alitaka kuwamiliki watoto pia kwa sababu alitaka warithi ardhi hiyo atakapoaga dunia. Mwanamume huyu hakutaka ardhi yake irithiwe na watu ambao hawakuwa wa ukoo wake. Hii ndio sababu iliyompelekea kutaka kuwa mtu wa pekee mwenye mahusiano ya kimapenzi na mkewe. Hali hii ndio iliyosababisha mahitaji ya mwanamke kuwa bikira kabla ya kuolewa. Kutokana na haya, ni wazi kuwa mahitaji ya mwanamke kuwa bikira yalianzishwa na wanaume ambao walikusudia kuendeleza mfumo wa ubabedume. Katika utenzi huu, Fatuma anasifiwa sana kwa kuwa bikira:

Wema wa Mwana batuli, binti Thumwa Rasuli,

Ukenea filhali, shariki na gharibia. (ubt 111)

Kitamani kwa kweli, kumwowaye batuli,

Alikihofu makali, kunena na Mursaa. (ubt 146)

Mwenye Ezi, Mfazali, akamba ndiyo ni kweli,

Ndoa ndakwe batuli, mwanamke mfazaa. (ubt 227)

Ubikira ni sifa inayomfanya Fatuma awavutie wanaume wengi. Sifa hii ya ubikira inasaidia kumsawiri mwanamke kama kiumbe wa pembeni (yaani kiumbe aliyehifadhiwa vyema, ametunza na kuhifadhiwa mahali fulani katika jamii ili asitangamane na ulimwengu unaoweza kumharibu). Huku ni kumgandamiza mwanamke.

**4:3 Hitimisho**

Katika sura hii, tumeshughulikia matumizi ya lugha na kuonyesha jinsi yanavyochangia kuikuza mada yetu ya upembezwaji wa mwanamke. Aidha tumeonyesha namna mbinu za ishara na sitiari zinavyochangia kumpembeza mwanamke katika utenzi huu.

Katika sura inayofuata, tutatoa mahitimisho ya utafiti wetu.

## SURA YA TANO

### MAHITIMISHO

Katika sura hii, tutatoa mahitimisho ya utafiti wetu. Utafiti huu ulishughulikia upembezwaji kama udokezi wa nafasi ya mwanamke katika *Utenzi wa Fatuma.* Nadharia tuliyoitumia katika utafiti huu ni ya ufeministi wa kirasimi. Nadharia hii ilifaa sana katika uhakiki wetu kwa kuwa imethibitisha kuwa ubabedume ndio sababu kuu ya kupembezwa kwa mwanamke katika *Utenzi wa Fatuma.* Asasi za ndoa, dini, elimu na utamaduni huchangia pakubwa kuhalalisha mfumo wa ubabedume.

Katika sura ya kwanza, tumeshughulikia maswala ya kimsingi yanayojenga utafiti wetu kama vile: kutambulisha utafiti, sababu ya kuchagua mada, tatizo la utafiti, madhumuni ya utafiti, nadharia tete, malengo ya utafiti, msingi wa kinadharia, upeo na mipaka, yaliyoandikwa kuhusu maada yetu na njia za utafiti tulizotumia.

Nadharia tete yetu ya kwanza katika utafiti huu ilikuwa; mwanamke amepembezwa katika utenzi wa Fatuma.Ya pili ilikuwa; ubabedume ndio sababu kuu ya kupembezwa kwa mwanamke katika *Utenzi wa Fatuma.* Nadharia tete yetu ya mwisho ilikuwa; matumizi ya lugha katika utenzi wa Fatuma yanachangia kupembezwa kwa mwanamke. Katika sura ya pili, ya tatu na ya nne, tumezitathimini kwa kina nadharia tete hizi kama njia ya kuthibitisha mada yetu.

Katika sura ya pili tulishughulikia ubabedume kama mhimili mkuu wa upembezwaji wa mwanamke. Tulishughulikia mfumo wa ubabedume kwa kuwa ndio uliokuwa msingi wa uhakiki wetu wa *Utenzi wa Fatuma* katika sura ya tatu. Tulieleza historia ya ubabedume kwa kuwa uelewa wa historia hii ulituwezesha kuelewa jinsi asasi za ndoa, dini na utamaduni zinavyochangia kupembezwa kwa mwanamke katika *Utenzi wa Fatuma.*

Katika sura ya tatu, tuliuhakiki *Utenzi wa Fatuma* kwa kutumia nadharia ya ufeministi wa kirasimi. Tulionyesha ufaafu wa nadharia hii katika kuuhakiki utenzi huu. Tulithibitisha kuwa asasi za ndoa, dini na utamaduni zinachangia pakubwa kupembezwa kwa mwanamke katika *Utenzi wa Fatuma.*

Tulionyesha kuwa mwanamke katika utenzi huu amepembezwa kwa kutohusishwa katika shughuli za posa. Wanaume kutoka maeneo mengi duniani wanataka kumwoa Fatuma kwa kuwa sifa za uzuri wake wa tabia na urembo wake zilikuwa zimewafikia. Wanaume hawa wanafika nyumbani kwa Mtume Muhammad kumposa Fatuma. Wengine wao wanatuma wajumbe kwa Mtume Muhammad kumposa Fatuma kwa niaba yao. Kati ya watu hawa kuna matajiri na wafalme kutoka maeneo mbalimbali. Watu hawa wote hawafanikiwi kumwoa Fatuma. Ali ndiye anayefanikiwa kumwoa Fatuma hatimaye. Hata hivyo, shughuli hizi za ndoa zinaendelea bila ya kuhuzishwa kwa Fatuma.

Baada ya posa ya Ali kukubaliwa na Mungu mbinguni, maandalizi yanaanza kufanywa huko mbinguni na malaika. Baada ya maandalizi haya ndoa kati ya Ali na Fatuma inaandaliwa

mbinguni. Mungu anamwakilisha Fatuma naye malaika Jibrili anamwakilisha Ali. Malaika Mikaili ndiye aliyekuwa shehe wa kuiunganisha ndoa hii. Fatuma hahuzishwi katika ndoa hii. Aidha, malaika Mikaili anapoenda duniani kupeleka habari hizi za ndoa kati ya Ali na Fatuma, Mtume Muhammad ndiye anakuwa wa kwanza kujulishwa kuhusu ndoa hii. Tunatarajia kuwa malaika huyu angempasa Fatuma habari hizi kabla ya kumpasa babake kwa sababu ndiye anayeolewa. Kinyume na matarajio haya, Fatuma anakuwa mtu wa mwisho kupaswa habari hizi zinazohusu ndoa yake.

Mtume Muhammad anapoenda kumjulisha Fatuma kuwa Mungu alikuwa amemteua Ali kuwa muwewe, anamjulisha pia kuhusu mahari yaliyokuwa yameletwa na malaika kutoka mbinguni. Fatuma hayakubali mahari hayo lakini anakubali kuolewa na Ali. Fatuma hahuzishwi katika maamuzi kuhusu kiwango cha mahari kitakachotolewa. Aidha malaika wanapowasili duniani na mahari hayo kutoka mbinguni, hawampelekia Fatuma moja kwa moja, wanaenda kwa Mtume Muhammad kwanza. Fatuma hahuzishwi moja kwa moja.

Mwanamke amepewa jukumu la kuwalea watoto. Mkewe Mtume Muhammad alipoaga dunia, Mtume alihuzunika sana. Aliona kuwa alikuwa amepoteza mlezi wa watoto wake. Mwanamume hashiliki katika kazi ya kuwalea watoto. Jukumu hili muhimu liwewachiwa mwanamke. Mwanamume ana uhuru wa kutoka na kuingia nyumbani apendavyo. Lakini mwanamke anabaki nyumbani na kuendelea na kazi ya kulea watoto na kazi nyingine za nyumbani. Mtume Muhammad anapoenda kuswali msikitini, Fatuma anaachwa nyumbani.

Uhakiki wetu wa *Utenzi wa Fatuma* unathibitisha kuwa asasi za dini, ndoa na utamaduni zinachangia kupembezwa kwa mwanamke katika utenzi huu. Asasi hizi zinafanya hivi kwa sababu zinachangia kuuendleza mfumo wa ubabedume ambao ni mhimili mkuu wa upembezwaji wa mwanamke.

Katika sura ya nne, tulishughulikia matumizi ya lugha katika *Utenzi wa Fatuma.* Tulionyesha jinsi matumizi hayo ya lugha yanavyochangia kujenga maudhui ya upembezwaji wa mwanamke katika utenzi huu.

Utafiti huu umechunguza upembezwaji kama udokezi wa nafasi ya mwanamke katika *Utenzi wa Fatuma.* Tumeonyesha jinsi asasi za ndoa dini na utamaduni zinavyochangia kupembezwa kwa mwamamke. Hata hivyo, hatujabainisha wazi asasi inayochangia zaidi kupembezwa kwa mwanamke katika ya asasi tulizoeleza. Tunapendekeza kuwa watafiti wengine washughulikie mada hii kwa kuchunguza asasi inayochangia zaidi kupembezwa kwa mwanamke katika *Utenzi wa Fatuma.*

**Marejeleo**

Ahmadi, H.A ( 1971) *Kurani Tukufu.*(Toleo la pili) Lahore: Pakistan Printing Works.

Al-Marzouqui,I.A(2000) *Human Rights in Islamic Law*. U.A.E: Abu Dhabi Publishers.

De Beauvoir, S. (1949). *The Second Sex.* Chapa ya Picador Classics. (1988) London: Pan Books Ltd.

Ellimann (1968). *Thinking about women.* New York: Harcourt.

Friedan, B. (1963). *The Femine Mystique*. New York: Dell.

Gerda, L(1986) *The Creation of Patriachy*. New York: Oxford University Press.

Girling, D.A(mhariri) (1978) *Everyman's Encyclopaedia*. Great Britain: J.M Dent & Sons Ltd.

Humphries, C (mhariri) (2002) *Philip's Encyclopedia*. London: George Philip Limited.

Iqbal,M (1989) *The Virtues of Women*. Vermont: Amana Books.

Khatab, H (1993) *The Muslim Woman`s Handbook.* London: Ta – Ha Publishers Ltd.

Lugano, R.S (1989) *Mwanamke Katika Riwaya za Kezilahabi.* Tanifu ya M.A. Chuo Kikuu Cha Nairobi. Haijachapishwa.

Maina, V. (2005). *Nafasi ya Mwanamke katika Tenzi mbili za Shaaban Robert : Utenzi wa Hati na Utenzi wa Adili* .Tasnifu ya M.A. chuo kukuu cha Nairobi : Haijachapishwa.

Maududi, S.A (1974) *Purdah and the Status of Women in Islam*. Delhi:Markazi Maktaba Islami.

Mernissi, F (1987) *Women and Islam: An Historical and Theological Enquiry*. Oxford: Blackwell Publishers Ltd.

Millet, K. (1969). *Sexual Politics.* London: Virago

Moi, T. (1985). *Sexual / Textual Politics*. USA : Methuen & Co. Ltd.

Momanyi, C. (1998). *Usawiri wa Mwanamke Mwislamu Katika Jamii ya Waswahili inavyobainika katika Ushairi wa Kiswahili.* Tasnifu ya Ph.D Chuo Kikuu Cha Kenyatta. Haijachapishwa.

Mutua, J.M(2007) *Mitazamo ya Vijana na Wazee Kuhusu Ukombozi wa Mwanamke Katika Tamthilia Tatu za Kiswahili*. Tanifu ya M.A. Chuo Kikuu Cha Nairobi. Haijachapishwa.

Ndungo, C. M. (1985). *Wanawake na Mabadiliko ya Kihistoria katika Fasihi ya Kiswahili.* Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Nyaberi, H.M(1997) *Mwamko wa Mwanamke Katika Tamthilia nne za Penina Muhando.* Tanifu ya M.A. Chuo Kikuu Cha Nairobi. Haijachapishwa.

Safra, J.E(mwenyekiti wa halmashauri) (2003) *The New Encyclopaedia Britannica*. London:

Britannica Inc.

Schimmel, A (1997) *My Soul is a Woman:The Feminine in Islam*. New York: The Continuum International Publishing Group Inc.

Seif – al – Hatimy, S.A (1979) *Women in Islam: A Comparative Study*. Lahore: Islamic Publications (pvt) Ltd.

Siddiqi, M.S (1982) *The Blessed Women of Islam*. Lahore: Kazi Publications.

Swaleh,A (1992) *Maudhui katika Utenzi wa Mwana Kupona*. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu Cha Nairobi. Haijachapishwa.

TUKI(2004) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi. Misingi na Vipengele Vyake.*Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

------------------ (2003) *Kamusi ya Fasihi*: Istilahi na Nadharia.Nairobi: Focus Books.

Wandera, S.P(1996) *Usawiri wa Mwanamke Katika Ushairi wa Kiswahili: 1800 1900:Uhalisi au Ugandamizwaji?* Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu Cha Egerton.

Wollstonecraft, M. (1962). *A Vindication of the Rights of Women.* Harmondsworth. Penguin Books.

Woolf, V. (1929). *A Room of One's Own.* London: The Hugarch Press

Zeba, S(1976) *A Guide for Muslim Parents Living in North America*. Maryland: Interational Graphics Printing Service.